# Nipashe

Jumanne Julai 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580997 *

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SportPesa

JACKPOT BABA LAO!

TZS. 274,002,680


CHEZA SASA KWA 1000/= TU!

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#


TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

**Watakaotoa** siri taarifa Sensa ya Watu na Makazi kufungwa

UKURASA 7




RASHFORD ATAKA MWANZO MPYA

UKURASA 22

# Samia: Siridhishwi hali bandarini, siasa zimejaa

• **Amtumbua** Mkurugenzi, amteua... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali baada ya kushuhudia utiaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha nne kutoka Tabora-Isaka Km165 katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**PSSSF YAWEKEZA TRIL. 7.6/- MIRADI**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umewekeza Sh. trilioni 7.6 kwenye miradi...

UKURASA WA 5

**ALIYEKUWA MKURUGENZI TPA ASOMEWA MASHTAKA KITANDANI**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Madeni Kipande (66)...

UKURASA WA 7

**SEKTA BINAFSI YATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA KIBIASHARA**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa sekta binafsi za ndani ya nchi kuchangamkia fursa za...

## Neema wastaafu NSSF kulipa mafao bil. 648/- mfuko wakadiriwa thamani tril.6/-

UKURASA 3

## Wananchi walalamika vigogo kupendelewa viwanja

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, YANGA CHALI KWA SOPU UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam kutoka Lisbon nchini Ureno alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano wa pili wa Umoja wa Mataifa kuhusu Uhifadhi wa Bahari na Rasilimali zake. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Samia: Siridhishwi hali bandarini, siasa zimejaa

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema haridhishwi na utendaji kazi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na kuwataka kubadilika kufanya kazi kwa bidii na kuacha siasa.

Alisema serikali inafanya kazi kubwa ya kuiunganisha nchi na fursa za kibiashara, lakini inakwamishwa na utendaji wa bandari hiyo.

Rais Samia alitoa karipio hilo jana, Ikulu, jijini Dar es Salaam katika hafla ya utiaji saini wa mikataba miwili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha nne Tabora hadi Isaka, yenye urefu wa kilometa 165 kati ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Kampuni za Yape Markez na Korail.

"Wale tuliowakabidhi uendeshaji wa bandari zetu wafanye kazi kwa kasi mno, siridhishwi kabisa na kasi za bandari, siasa zilizoko, longolongo zilizoko. Watu huko nje (nje ya nchi) bandari zinaendeshwa kwa kasi kubwa.

"Wawekezaji wanakuja ni kuzungushwa mwanzo mwisho, tutizame siasa, tutizame uchumi. Nasema bandari watu wafanye kazi, kwa hiyo tutatupia jicho vizuri katika masuala ya bandari. Wale waliokabidhiwa bandari nataka tuelewane vizuri," alisisitiza Rais Samia.

Alisema kuwa ujenzi mkubwa umefanyika katika bandari hiyo kwa kuwa ni lango na fursa kubwa ya kuunganisha baadhi ya nchi za Bara la Afrika na Asia zenye uchumi unaokua kwa kasi duniani.

"Kwa hiyo kama nilivyosema bandari hii ndiyo jicho letu. Na bandari hii ikifanya kazi vizuri nusu ya bajeti tunayoipanga kila mwaka itatolewa ndani ya Bandari ya Dar es Salaam. Kwahiyo niwaombe sana wale wa bandari wakae vizuri twende tukafanye kazi kwa kasi," alisema.

Kuhusu mkataba uliosainiwa, Rais Samia alisema kuwa ujenzi wa reli hiyo ukikamilika utasaidia kuunganisha mikoa tisa ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Simiyu, Sinyanga na Mwanza. Vilevile, itaiunganisha Tanzania na nchi za Uganda, Burundi, Rwanda, DRC na Sudani ya Kusini pamoja na nchi nyingine hapo baadaye.

Mradi huo, alisema ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na ajenda ya 63 ya nchi za Umoja wa Mataifa (AU) inazozitaka kujenga reli ya kati kuzunguka nchi zote za Afrika ili kukuza biashara.

Alisema, kukamilika kwa reli hiyo kutatimiza lengo la serikali la kuifanya miji mikuu ikiwamo Dar es Salaam, Mwanza na Tabora kuwa kitovu cha biashara Afrika na kuunganisha na miji mingine ya kibiashara ndani ya bara hilo.

"Sasa kwa hapa kwetu (Tanzania) tumaini la reli ni kuunganisha mji mkuu wa Dar es Salaam. Kama mnavyojua lengo letu ni kuifanya Dar es Salaam kuwa kitovu cha biashara ndani ya Afrika. Kwahiyo tukiweza kuungwa vizuri Dar es Salaam inakwenda kukua," alisema.

**AMTUMBUA MKURUGENZI**

Saa chache baada ya Rais kueleza kutoridhishwa na bandari, taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu, Zuhura Yunus, ilieleza kumtumbuliwa kwa Mkurugenzi wa Bandari, Eric Hamisi na nafasi hiyo kuchukuliwa na Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Plasduce Mbosa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema mkataba wa kwanza uliosainiwa kati ya TRC na kampuni ya Yape Markez ni wa ujenzi wa kipande hicho kwa miezi 42 utakaogharimu Sh. trilioni 2.094 pamoja na majaribio.

Huku mkataba wa pili kati ya shirika hilo na kampuni ya ujenzi wa reli ya Korail utahusisha kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wataalamu wa Kitanzania kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi huo.

Alisema kipande hicho kitakuwa na kituo cha abiria na mizigo katika maeneo ya Zubuka na Bukene, pamoja na kujengwa chuo kikubwa cha kufundishia Watanzania.

"Katika kipande hiki tunachosaini tutajenga chuo kizuri sana pale Tabora. Chuo kizuri cha kufundishia watu wetu. Na tutakuwa na kituo kikubwa sana cha mizigo pale Tabora kwa sababu pale ndio treni zote zinakutana," alibainisha.

Pia alisema kutajengwa karakana kwa ajili ya matengeneza ya treni Tabora. Huku mradi huo ukizalisha ajira kwa watu 16,000 zenye thamani ya Sh. bilioni 224 na zabuni zenye thamani ya Sh. trilioni 1.776 zimetolewa kwa makandarasi na wazabuni 1,663.

## Wananchi walalamikia vigogo mgawanyo viwanja

**Na Richard Makore,** MWANZA

BAADHI ya wananchi walioomba kuuziwa viwanja eneo la Luchelele na Isamilo, jijini Mwanza, wamelalamika kukosa viwanja hivyo na kudai viongozi wa serikali na wabunge kuviwahi.

Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilitangaza kuuza viwanja hivyo na kuwataka wanaovitaka kuchukua fomu kuanzia Juni 2 hadi 6, mwaka huu.

Wakizungumza na gazeti hili, walidai waliomba viwanja hivyo baada ya kujaza fomu na kukamilisha malipo ya maombi ya Sh. 20,000, lakini orodha iliyotoka ina majina ya vigogo.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza na kuwekwa kwenye tovuti yao ina orodha ya watu 427 waliopata eneo la Luchelele na 39 Isamilo.

Majina ya vigogo yalijitokeza kwenye viwanja vya Isamilo ni ya Spika wa Bunge Tulia Akson, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), Alphayo Kidata, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mery Masanja.

Wengine ni Mbunge wa Nyamagana, Stanslaus Mabula, Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Seleman Yahaya na Meya wa Jiji hilo, Sima Costantine Sima na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Ngusa Samike.

Wengine ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, Michael Magufuli na Mkuu wa Mkoa mstaafu, Said Meck Sadik, ambao wengi wamepewa viwanja eneo la Isamilo ambalo lipo katikati ya Jiji la Mwanza.

Fedha za kuchukua fomu zilikusanywa na Jiji la Mwanza huku wananchi wa kawaida wakijitokeza kulipia ili waweze kupata viwanja vya makazi na biashara.

Kwa mujibu wa tangazo hilo la kuwapatia viwanja vigogo hao, walitakiwa kufika ofisi za jiji kuchukua ankara ya malipo ili wakavilipie.

Mmoja wa wananchi walioomba kununua viwanja hivyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alidai alilipia benki Sh. 20,000 kwa ajili ya kuomba kiwanja eneo la Luchelele.

Vile vile, tangazo lililotolewa kwa wananchi wakati wa kutangaza kuuza viwanga hivyo, Luchelele mita moja ya mraba ilikuwa ikiuzwa Sh. 5,000 kwa viwanja vya makazi.

Eneo la Isamilo mita moja ya mraba ilikuwa ikiuzwa Sh. 25,000.

Katika maeneo hayo mawili pia alisema kulikuwa na viwanja kwa ajili ya makazi na biashara.

Tangazo la Jiji la Mwanza lilisema watu waliopatiwa viwanja hivyo walitakiwa kwenda kuchukua ankara za malipo kuanzia Juni 23 hadi Juni 30, mwaka huu.

Aidha, tangazo hilo ambalo lipo kwenye tovuti hiyo, lilisisitiza kuwa mtu yeyote atakayeshindwa kuzingatia muda huo atanyang'anywa kiwanja na kumpatia mtu mwingine.

Alipoulizwa kuhusu vigogo hao kupatiwa viwanja, Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Seleman Yahaya alisema amtumie ujumbe mfupi wa simu na kisha kukata simu.

Hata hivyo, ujumbe huo haukujibiwa.

# PM asema bilioni 2/- zitatekeleza miradi

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imetoa zaidi ya Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Kata ya Nanganga wilayani Ruangwa ikiwamo ya afya, elimu na maji.

Aliyasema hayo jana akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi hiyo kuwa serikali imetoa Sh. milioni 447 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa usambazaji maji Nanganga, Sh. milioni 31 ya kusambaza katika kijiji cha Mbecha na Sh. milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mchenganyumba.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya Shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa umwagiliaji Nanganga, tutumie vizuri bonde letu, vijana changamkieni fursa hii kwa kuanzisha kilimo cha mboga na mazao mengine," alishauri Majaliwa.

Aliuagiza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kuendelea na mpango wa ujenzi wa soko la mboga katika Kata ya Nanganga ili kuwawezesha wakulima wa mazao hayo kupata sehemu ya uhakika ya kufanyia biashara.

Alitoa wito kwa wanafunzi kujitahidi kusoma kwa bidii, na kuwa mbali na serikali kutoa elimu bure, pia imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya kutolea elimu nchini.

Diwani wa Kata ya Nanganga, Kambona aliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika kata hiyo ikiwamo wa usambazaji maji ambayo umetatua tatizo katika eneo hilo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi baada ya kukagua ujenzi wa Kituo cha Afya Nangumbu wilayani Ruangwa, akiwa katika ziara ya kikazi wilayani humo. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Neema NSSF kulipa wastaafu mabilioni

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amesema mfuko huo unakadiriwa kuwa na thamani ya Shilingi trilioni sita hesabu zinazoishia Juni 30, mwaka huu.

Mshomba alitoa taarifa hiyo katika Banda la NSSF kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), viwanja vya Julius Nyerere (maarufu Sabasaba) jijini Dar es Salaam.

"Thamani hiyo imekuwa ikikua sana kufuatia mwitikio mzuri wa uchangiaji ambao waajiri wamekuwa wakionyesha kwa takriban miaka miwili iliyopita," alisema na kuongeza; "Tunavyozungumza sasa hivi makusanyo ya mwezi yanazidi bilioni 110."

Alisema mwaka ulioishia Juni 30, NSSF ilikusanya zaidi ya Sh. trilioni 1.3.

"Hili ni ongezeko kubwa ukilinganisha na makusanyo ya mwaka uliopita ulioishia Juni 30 ambapo tulikusanya Sh. trilioni 1.1, ongezeko la zaidi ya asilimia 18, hii inatokana na kwanza kuwajengea mazingira mazuri ya kazi watumishi yanayopelekea kuongezeka kwa ari ya kufanya kazi, matumizi ya TEHAMA yanayoziba mianya ya utendaji kazi usio wa kuridhisha, mwitikio wa waajiri na wafanyakazi," alifafanua.

Alisema mfuko umekuwa ukiwapa waajiri elimu ya hifadhi ya jamii hatua ambayo anaamini imesaidia kuongeza tija.

Kadhalika, alisema kama mtu amewekeza NSSF mapato yake yapo, watoto wake watapata, mwenza atapata ndiyo maana Mfuko huo dhima yao ni kujali maisha ya mwanachama ya sasa na baadaye.

Kwa upande wa ulipaji mafao, alisema mwaka jana NSSF ililipa Sh. bilioni 594 na wanajiandaa kulipa Sh. bilioni 658 mwaka unaofuata ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 10.

**KODI YA SERIKALI**

Kwa upande wa serikali, alisema NSSF imekuwa ikisaidia kupitia ulipaji kodi katika miaka mitano iliyopita imelipa zaidi ya Sh. bilioni 400.

Pia mfuko huo unasaidia jamii kupitia (Corporate Social Responsibility) na kwamba kuna sera mahsusi inayowaelekeza kujikita katika mambo ya msingi kama vile afya, elimu, barabara na wanafanya kazi kubwa kupitia mpango huo.

Kuhusu ushiriki wa mfuko kwenye maonyesho hayo, alisema ni fursa nzuri ya kukutana na wadau ili kutoa elimu ya masuala mbalimbali yahusuyo hifadhi ya jamii na kuwahudumia wanachama na wananchi kwa ujumla.

"Tunatoa elimu ya kutosha kuhusu mabadiliko ambayo yametokea katika sekta ya hifadhi ya jamii kama mnavyofahamu kumekuwa na mabadiliko yanayohusu kanuni ya ulipaji pensheni, yaani namna ambavyo tunawalipa wastaafu wetu kuanzia tarehe 1/7/2022, tumebadilisha kidogo fomula ya ulipaji."

Alisema jambo hilo lilikuwa la muda mrefu tangu serikali ya awamu iliyopita mwaka 2018, yalitoka maagizo ya kulifanyia kazi suala hilo kwa kushirikisha wadau wa vyama vya wafanyakazi, waajiri na serikali.

Uamuzi huo wa serikali ni kufuatia malalamiko yaliyotokea baada ya fomula iliyowekwa kufuatia mabadiliko ya sheria ya mwaka 2018.

Alisema jitihada kubwa zilizofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, jambo hilo limewezekana na kuanzia tarehe hiyo kuna kanuni mpya ya ulipaji mafao.

"Kufuatia mabadiliko hayo NSSF sasa italipa malipo ya mkupuo asilimia 33 badala ya asilimia 25 ya kanuni ya zamani kwa hiyo ni jambo zuri na wanachama wamelipokea vizuri na maisha ya wanachama yataendelea kuboreka," alisisitiza.

Alisema mfuko huo unasisitiza matumizi ya mifumo TEHAMA, takriban miaka miwili unatoa kipaumbele shughuli zao kufanyika kwa kutumia mifumo.

"Ni jambo tulilolipa kipaumbele na tunatumia maonyesho haya kuzidi kuwaelimisha wanachama wetu na wananchi kwa ujumla kuhusu matumizi ya TEHAMA na tunawaahidi kwamba hata kwa zile shughuli chache ambazo hazijawekwa katika mfumo, ndani ya mwaka mmoja huu unaokuja tunatarajia tutakuwa tumeziweka," alisema.

HUDUMA SABASABA

Mkurugenzi Mkuu, alisema NSSF ipo kwenye maonyesho hayo kwa ajili ya kutoa huduma na pia mtu akija kuulizia michango yake, akitaka kujua hatua ya mafao yake yamefikia hatua gani aweze kulipwa.

**UWEKEZAJI**

Alisema NSSF ni moja ya taasisi kubwa nchini zinazowekeza kwa kiasi kikubwa na kutangaza uwekezaji kwenye nyumba zao za kupangisha na kununua.

Alitoa mfano wa nyumba wilayani Kigamboni hususan Mtoni Kijichi, Tuangoma, Dungu, maeneo ya Muongozo.

"Tuna nyumba nzuri sana na mwitikio wa kununua nyumba hizo umekua ni mzuri sana, pia tunajenga jengo la Mzizima hapa Dar es Salaam na nia hasa ni kulipangisha kwa watu watakaoendesha mradi wa hoteli pia Mwanza na lengo ni hilo hilo kulipangisha kwa mtu atakayeendesha shughuli za hoteli, tunatumia maonyesho haya kutangaza hizo nafasi ndani ya nchi, pia nje ya nchi ili tuweze kupata wadau hao ili kuhakikisha tunapata wapangaji au kununua nyumba hizo."


## BISMILLAH RAHMAN RAHIM



16928002

Familia ya marehemu **Dk. Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye Hitima ya kumuombea **Marehemu Dk. Omar Ali Juma** itakayofanyika siku ya Alhamisi tarehe **7 Julai, 2022 saa kumi jioni** katika **Msikiti Wa Ngazija**

Kufika kwenu ndio mafanikio yetu.

Ndugu, marafiki na jamaa wote mnakaribishwa.

**Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.**

**AMIN**

# PSSSF yawekeza tril. 7.6/- miradi

Na Mwandishi Wetu

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umewekeza Sh. trilioni 7.6 kwenye miradi mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Hosea Kashimba, alitoa taarifa hiyo jana katika banda la mfuko huo kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), yanayoendelea kwenye viwanja vya Julius Nyerere maarufu Sabasaba.

Alisema uwekezaji huo unarejesha asilimia nane. "Huu sio uwekezaji mdogo ni uwekezaji mkubwa na wenye tija."

Alisema baada ya uwekezaji huo mfuko una jukumu la kulipa mafao ya muda mrefu na muda mfupi.

"Ukijumlisha mafao yote haya tunalipa zaidi ya Sh. trilioni 1.6 kwa mwaka na kwa mwezi tunalipa pensheni Sh. bilioni 60, maana yake tunaingiza kwenye mzunguko wa uchumi wa nchi kwa hivyo utaona kuna mzunguko mkubwa wa fedha kwa wananchi na kuondoa umaskini ambao ungewakuta wananchi wetu kama wasingekuwa kwenye mpango wa Hifadhi ya Jamii."

Akifafanua kuhusu uwekezaji, Kashimba alisema mfuko umewekeza kwenye viwanda na kuvitaja kuwa ni pamoja na cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro International Leather Company Limited, pia mfuko unakamilisha ujenzi wa kiwanda cha machinjio ya kisasa, Nguru - Morogoro, kiwanda cha tangawizi Mamba Miamba, jimbo la Same, kwa kushirikiana na WCF katika uwekezaji wa kiwanda cha Cahi Mponde, Lushoto.

Alisema viwanda hivyo vitachachua uchumi wa nchi na kwa kufanya hivyo mfuko utakuwa umetekeleza azma ya serikali ya kutengeneza ajira kwa wananchi na kutoa mfano kuwa kiwanda kimoja kinaweza kuajiri wafanyakazi zaidi ya 3,000.

Kashimba pia alisema mfuko umewekeza kwenye majengo ya kisasa na yanayofaa (Real Estate) kwenye maeneo mbalimbali nchini.

"Kwa wawekezaji wanaotoka ndani na nje ya nchi tunawahakikishia kupata majengo mazuri yenye viwango kama nchi wanakotoka, tuna jengo zuri pale Sam Nujoma (PSSSF Commercial Complex), na lina eneo kubwa la kutosha, pia tuna majengo mengine katikati ya jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine," alisema Kashimba.




Msimamizi wa Huduma kwa Wateja wa kampuni ya kutoa mikopo kwa njia ya simu za mkononi kupitia App ya Branch, Reuben Wanyamawi, akiongea na wanahabari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mpango wa kampuni hiyo kuwafikia Watanzania wengi zaidi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya Sabaya yakwama tena

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUTOKAMILIKA kwa upelelezi na kukosekana kwa hati ya kuipa kibali Mahakama ya Hakimu Mkazi mamlaka ya kuisikiliza kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro Lengai Ole Sabaya na wenzake wanne, kumesababisha kesi hiyo kupigwa kalenda hadi Julai 14.

Shtaka hilo linawakabili Ole Sabaya, Silivester Nyagu, John Aweyo, Nathan Msuya na Antoro Assey.

Wakili wa utetezi, Helena Mahuna, aliomba mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, Salome Mshasha, Jamhuri kulichukulia suala hilo kwa umakini na kuharakisha ili kesi hiyo ianze kusikilizwa kama walivyodai awali ushahidi umekamilika.

Alidai kuwa, jana ni mara ya tatu kwa shtaka hilo kuahirishwa na kusababisha washtakiwa kuendelea kusota magereza bila kujua hatima ya kesi yao.

"Mheshimiwa hakimu hatuna shida na kutajwa kwa kesi hii, ila tunaomba wenzetu wa Jamhuri watambue wateja wetu wanateseka na wengine ni wagonjwa, wachukulie jambo hili kwa uzito zaidi katika kukamilisha taratibu zao," alidai.

Wakiomba kuahirishwa kwa kesi hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Kasimu Daudi, aliyeongozana na Sabikia Mcharo, walidai kuwa bado upelezi haujakamilika, kibali pamoja na hati ya kuipa mahakama hiyo uwezo wa kusikilizwa kwa shauri hilo.

Alidai kuwa wanaendelea kufanyia kazi malalamiko yanayotolewa na upande wa utetezi na kuongeza kuwa wapo makini na wanalichukulia kwa uzito mkubwa.

"Mheshimiwa Hakimu, shauri hili limekuja kwa ajili ya kutajwa siku ya leo (jana), upelelezi haujakamilika, kibali pamoja hati ya kuzipa mahakama hii mamlaka ya kusikiliza bado haijatolewa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP), kutokana na sababu hiyo tunaomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa, ili tufuatilie haya mambo yakamilike na tuendelee na shauri hili," alidai wakili upande wa Jamhuri.

Akiahirisha kesi hiyo, Hakimu Mshasha aliutaka upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi na kutafuta hati na vibali ili washtakiwa waweze kupata haki zao na kesi hiyo imeahirishwa hadi Julai 14, mwaka huu.

## Rais Mwinyi aridhishwa uboreshaji maonyesho DITF

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema maonyesho ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yameboreshwa zaidi.

Rais Mwinyi alitoa kauli hiyo jana baada ya kutembelea maonyesho hayo ambayo mwaka huu ni ya 46 yanayoendelea kwenye viwanja vya Sabasaba.

"Nimetembelea mabanda katika maonyesho haya, inatia moyo kuona kila mwaka yanaboreshwa zaidi," alisema Rais Mwinyi.

"Kikubwa zaidi nimeoma wajasiriamali wetu wameboresha bidhaa, vifungashio. Hii inadhihirisha kwamba taasisi zetu zinafanya kazi nzuri kuhakikisha bidhaa zinaongezewa thamani."

Alisema serikali itahakikisha kwamba inaendelea kuboresha mazingira ya biashara ili wafanyabiashara na wawekezaji wafanye kazi zao kwa urahisi.

"Tunataka hata upatikanaji wa vibali kwa wawekezaji wetu ufanyike kwa uharaka na mufa mfupi," alisema Rais Mwinyi.

Kwa upande wake, Waziri wa Viwanda na Uwekeji, Ashatu Kijaji, alisema wameandaa kliniki ya biashara ambayo itajumuisha wafanyabiashara wote lengo ni kutaka wajifunze mambo mbalimbali ikiwamo kiboresha zaidi uzalishaji wa bidhaa.



# Aliyekuwa Mkurugenzi TPA asomewa mashtaka kitandani

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Madeni Kipande (66), amesomewa mashtaka matatu ya uhujumu uchumi akiwa kitandani katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Kitengo cha Mifupa (MOI), baada ya kufanyiwa upasuaji wa mgongo.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, ilihamia kwa muda jana katika hospitali hiyo kwa ajili ya kumsomea Kipande mashtaka yanayomkabili kuanzia saa 8:57 hadi saa 9:08 mchana, likiwamo la kuisababishia TPA hasara ya Sh. bilioni 4.2.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Timotheo Mmari mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalira, alidai kuwa katika shtaka la kwanza Kipande na wenzake wanne walikula njama ya kutenda kosa la kuisababishia TPA hasara kati Oktoba Mosi, 2014 na Oktoba Mosi, 2020, jijini Dar es Salaam.

Wenzake ni Peter Gawile (58) Ofisa Rasilimali Watu wa TPA, Casmily Lujegi (65) na Mwenyekiti wa Bodi ya Manunuzi wa TPA, Mashaka Kisanta (59) Mkurugenzi wa Idara ya Manunuzi na Kilian Chale (51), Kaimu Mkurugenzi Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, wote wakazi wa Dar es Salaam.

Alidai kati ya Januari Mosi, 2015 hadi Februari 17, mwaka 2015, washtakiwa wakiwa maofisa wa TPA, walitumia madaraka yao vibaya kwa kutangaza zabuni namba AE/016/2014-15/CTB/G/39 kwa nia ya kujipatia Dola za Kimarekani 1,857,908.04.

Mmari alidai kati ya Oktoba Mosi 2014 na Oktoba Mosi, 2020 maeneo ya TPA na maeneo mengine ya Dar es Salaam, washtakiwa kwa makusudi walitangaza zabuni ya Enterprises Planning Resources (ERP).

Ilidaiwa walitangaza zabuni hiyo, bila kupata kibali cha bodi ya zabuni ya mamlaka hiyo na kushindwa kufuata kanuni kwa kutoa malipo ya awali ya asilimia 40 bila idhini ya bodi hiyo, jambo lililoisababishia TPA hasara ya Dola za Kimarekani milioni 1.8 (Sh. bilioni 4.2).

Hakimu Rugemalira alimweleza mshtakiwa hatakiwi kujibu chochote kwa sababu Mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi hadi itakapopata kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Pia Hakimu Rugemalira alimweleza kwamba kiasi kilichotajwa dhamana yake inaomba Mahakama Kuu na alipowauliza Wakili Mmari kuhusu upelelezi alidai bado haujakamilika.

Hata hivyo, Kipande akiwa kitandani kwa sauti ya chini, aliuliza utaratibu wa kesi ikifunguliwa upelelezi unatakiwa uwe umekamilika, akidai yeye sio mwanasheria ameuliza tu.

Hakimu Rugemalira alimweleza kwamba ni kweli kuna mabadiliko ya sheria yamefanyika kwamba kesi hailetwi mahakamani hadi upelelezi ukamilike, lakini kuna mashtaka yametajwa kwenye hiyo sheria kuwa yanaweza kuletwa kabla ya upelelezi kukamilika yakiwamo mashtaka yanayomkabili.

Kipande alihoji pia atawezaje kwenda Mahakama Kuu kufuatilia dhamana kwa hali yake na Hakimu alimweleza kuwa sio lazima aende yeye amtafute wakili atamwakilisha.

Huku akionyesha tabasamu, Kipande alidai mawakili wana bei kubwa. "Nategemea haki inatendeka na wapelelezi watafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria bila kula rushwa kwa sababu makosa mengine ni ya kubambikiwa," alidai.

Hakimu alimweleza maelezo hayo atayatoa wakati wa ushahidi na pia aliimwambia washtakiwa wenzake wapo Keko Gerezani, walisomewa mashtaka yao Juni 30, 2022.

Hakimu Rugemalira aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 14, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

# Branch yajivunia miaka 12 mikopo wajasiriamali

**Na Frank Monyo**

TAASISI ya Branch, inayojihusisha na utoaji mikopo wa njia ya simu ya mkononi imetaja kundi la wajasiriamali kuongoza kukopa katika taasisi hiyo kwa kipindi cha miaka 12, tangu kuanzishwa kwake nchini kwa lengo la kukuza biashara zao.

Taasisi hiyo iliyoanza shughuli zake nchini mwaka 2015 imeeleza kuwa mpaka Julai mosi, mwaka huu, imewafikia watu milioni 1.5 na kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 73.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, wakati akijitambulisha kwa wahariri na waandishi wa vyombo vya habari, Msimamizi wa huduma kwa wateja kwa Tanzania, Reuben Wanyamawi, alisema Branch imejipanga vyema kuwafikishia huduma za mikopo Watanzania popote pale walipo na muda wowote.

"Wateja wengi ambao tunawapata ni wafanyabiashara wadogo, kwa mfano leo tutakutana na mteja mmoja, ambaye anafanya biashara ndogo na ametoka mbali na sisi alianza kukopa Sh. 10,000 alikuwa anafanya biashara ya samaki hadi sasa anaweza kukopa zaidi ya Sh. 200,000," alisema Wanyamawi na kuongeza:

"Ukiona hiyo stori, sisi inatupa furaha kubwa sana na ndiyo maana nataka kumuona mteja wetu, kwani hawa wajasiriamali ndiyo wanaokuza jina la Branch na sisi tunapenda kuwasapoti ili kuwainua," alisema.

Alisema kuwa mikopo ya taasisi hiyo inatolewa kupitia App yao inaanzia kiasi cha Sh. 5,000 hadi Shilingi milioni moja.

"Tunaamini kuwa kila mtu popote pale alipo anahitaji na anastahili huduma za kifedha. Kuongezeka kwa matumizi ya simu janja kunaongeza fursa kwa watu wengi zaidi kufikiwa na huduma za kifedha," alisema.

IITA
Transforming African Agriculture
ILRI

## POSITION ANNOUNCEMENT
## HERD HEALTH FIELD COORDINATOR
### IITA-TZ-2022 - R4D-008 -NRS-DSM

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Livestock Research Institute (ILRI) invites applications for the position of Herd Health Field Coordinator. The Herd Health Field Coordinator will contribute to research for development of livestock value chains in Tanzania under the One CGIAR "Sustainable Animal Productivity for Livelihoods, Nutrition and Gender Inclusion" (in short, "SAPLING") Initiative implemented by ILRI, ICARDA and ABC- CIAT. SAPLING aims to enable 800,000 livestock producers – especially women and youth in 7 countries to engage in inclusive value chains and achieve sustainable productivity gains resulting in improved livelihoods.

Tanzania is one of seven focus countries identified as a priority given the importance of livestock in the livelihoods of its people and the commitment of public and private actors to transform food systems through sustainable livestock development. Smallholder dairy and poultry value chains have been selected as priority value chains in the country under the Initiative.

The Herd Health Field Coordinator will principally focus on piloting of integrated herd health initiatives in smallholder dairy, building on Maziwa Zaidi activities to catalyze enhanced uptake of proven dairy technology packages in pilot sites in Kilimanjaro and Tanga regions. The technology packages include delivery of bundled vaccine and artificial insemination services through inclusive business models involving empowered women and youth agripreneurs. Usage of information communication technology (ICT) or digital tools including mobile smartphone applications for farmer profiling and e-extension is envisaged.

Duty Station: This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Dra es Salaam , Tanzania

**Key accountabilities**

- Coordinate herd health field research activities in Tanzania under SAPLING Initiative
- Lead implementation of herd health monitoring, learning and evaluation including questionnaire design and epidemiological data collection
- Lead preparation of herd health reports and communication products from field activities
- Establish and manage client and stakeholder relationships
- Contribute to publishing results of research
- Maintain project work plan
- Verify and analyse the accuracy of data and information used or generated by project partners; resolve any discrepancies or problems.
- Propose ideas to the project team for improving the implementation of the project based on experience on the ground
- Prepare records of project activities and ensure the timely processing and delivery of required reports

**Academic requirements**

Bachelor's degree in veterinary medicine and MSc in epidemiology, agribusiness, project management, economics or rural development

**Specific experience required**

- A Tanzanian in mid-career with at least 6 years' work experience; a minimum of 3 years of which should have been spent in the delivery of development projects working with an NGO or in the private sector
- Awareness and/or experience in use of digital ICT tools by animal health practitioners including Mobile apps
- Field experience in livestock (preferably dairy) R4D in Tanzania – especially in linking farmers to inputs and services
- Experience with supervising/coordinating collection, storage and analysis of data related to agricultural households and associated value chains. Strong data analytical skills and knowledge of statistical applications such as using 'R', STATA or SPSS.
- An understanding of innovation systems and entrepreneurship
- Proven experience with project planning, management and monitoring & evaluation.
- Problem solving skills
- Excellent leadership skills
- Excellent written and spoken English and Swahili

**General information:**

The duration of contract for the position is two years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, **IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania** or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope.

**Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

216928502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mazingira yanaharibiwa, ukataji miti washamiri

**MABADILIKO** ya tabianchi kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na uharibifu wa mazingira unaofanywa na binadamu.

“Ulinganisho ni rahisi, kama tukilinda misitu yetu nayo itatulinda. Kama tukiharibu misitu yetu tunajiharibia wenyewe.” Ni kauli ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres aliyoitoa Julai 2, nchini Suriname.

Kauli hiyo inatukumbusha kuwa binadamu na mimea tunategemeana kwa kiasi kikubwa, zaidi sisi binadamu tunaitegemea mimea kwa maisha yetu kuanzia kutupatia hewa safi, mvua na chakula.

Hata hivyo, binadamu wamekuwa waharibifu wakubwa wa misitu kwa kuikata na kusababisha nchi nyingi kugeuzwa majangwa na kilio cha mabadiliko ya tabianchi.

Nchi zinakosa mvua za kutosha kwasababu hakuna miti, upungufu wa chakula unatishia dunia kwasababu ya mabadiliko ya tabianchi na hali hii chanzo chake kinasababishwa na binadamu.

Ripoti mpya ya Shirika la Utabiri wa Hali ya Hewa Duniani (WMO) iliyotolewa mwezi Machi, 2019 inasema majanga ya asili, ikiwamo mafuriko, vimbunga, joto la kupindukia, kuongezeka kwa kina cha bahari na matukio kama elnino, vyote vinaongezeka kutokana na mabadiliko haya ya tabianchi na hali inatarajiwa kuwa mbaya zaidi endapo hatua madhubuti hazitochukuliwa.

Hapa nchini mabadiliko ya tabianchi yameanza kuonekana kutokana na baadhi ya mikoa ambayo ilizoeleka katika kipindi fulani kuwa na mvua nyingi, sasa hivi zinakosa matokeo yanayosababisha kukosekana kwa chakula cha kutosha na tishio la njaa.

Elimu inatolewa mara kwa mara kuhusu athari za uharibifu wa mazingira zinazosababisha mabadiliko ya tabianchi, lakini watu wanaohusishwa na uharibifu huo wameonekana kuziba masikio huku wakiendeleza hali hiyo.

Ukipita barabara inayoelekea Mkoa wa Pwani, unaweza kupigwa na butwaa jinsi wafanyabiashara wa mikaa wanavyojaza magunia kwenye malori na pikipiki kwa ajili ya kwenda kuuza mijini hasa Jiji la Dar es Salaam.

Ukipiga hesabu kwa siku si chini ya magari 10 na pikipiki 20 zinazosafirisha bidhaa hiyo ya mkaa kwenda mjini.

Ukiangalia idadi hiyo ya magunia utagundua jinsi gani misitu inavyoteketezwa na kuhatarisha nchi kugeuzwa jangwa.

Hali hii ya ukataji misitu inaathiri pia wanyama wanaotegemea chakula chao kutoka kwenye misitu hiyo.

Wafugaji wanalalamika mifugo yao kukosa chakula na kulazimika kuihamisha kutafuta sehemu zenye malisho ili isife njaa.

Baadhi ya wafugaji hao wamegeuka kuwa walinzi wa misitu isikatwe, lakini waharibifu hao wakigundua kuwa wanafuatiliwa, hugeuza muda wa kukata miti ambao hufanya mchana na sasa kukata usiku.

Wafugaji wanapopitisha mifugo yao kwa ajili ya kuwapa malisho hukuta tayari uharibifu umeshafanyika na kukosa njia nyingine ya kuwadhibiti.

Kama kungekuwa na ushirikiano wa kutoka kwa viongozi wa vijiji wa kudhibiti wahalifu hao, ukataji misitu ungedhibitiwa.

Lakini baadhi ya viongozi wanatuhumiwa kuhusika kuwaruhusu wahalifu hao kukata miti kwa kupokea kitu kidogo, bila kujali kuwa hali hiyo inaleta athari kubwa kwa nchi na vizazi vijavyo kwa nchi kugeuzwa jangwa.

Kwa pamoja wanaofanya biashara hiyo bila kibali cha mamlaka wakidhibitiwa na wengine wataogopa kwa sababu watajua sheria itachukua mkondo wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Madai biashara baa kunyanyasa mabinti kingono yatazamwe

**BAADHI** ya maeneo yanayotajwa kunyanyasa wasichana (mabinti) chini ya miaka 18 ni sehemu zinapouzwa pombe.

Baa nyingi mijini hasa kwenye majiji kunafunguliwa baa kila wakati na wateja wanajaa. Mathalani, jijini Dar es Salaam, zama hizi licha ya watu kudai kuwa maisha ni magumu lakini yaelekea si magumu kwenye pombe. Kila mahali baa zimejaa.

Kinachoshangaza na wengi kujiuliza ni hiki inakuwaje baa zinajaa kiasi hiki hasa mpya ambazo ni kama zimesambaa kila kwenye barabara kuu au zile za mitaani zinazotumiwa na watu wengi.

Madai ni kwamba hao wanaoitwa wateja wengi wanachofuata ni wasichana au mabinti ambao wanadaiwa kuwa hutumiwa kuvuta wateja na hata kukuza mauzo ya vinywaji na vyakula katika baa nyingi za mijini.

Yapo madai kuwa wasichana hao hubadilishwa kila baada ya kipindi fulani inaweza kuwa miezi mitatu au sita ama mmiliki wa baa au meneja anavyopenda.

Baadhi ya mabinti hao wanadai kuwa hunyanyaswa wakati wa kazi na kuna baadhi ya wamiliki hawawalipi mishahara badala yake huwalazimisha kuwa na uhusiano na wateja na kwa kifupi huwataka kujiuza kwa wateja.

Inaonekana kuwa pengine ni mkakati wa baadhi ya wafanyabiashara au mameneja wa baa kuwatumia wasichana hao ili kuuza mauzo zaidi au kama moja ya mbinu ya kukuza biashara zao.

Wasichana hao wa baa huvalishwa mavazi mafupi kuonyesha miili yao lakini hutumikishwa kufanyakazi muda wote na uzuri wao au sura nzuri na maumbile yao ndiyo kinachogeuzwa mtaji kwa wauza pombe.

Lakini jambo jingine ni madai ya wasichana hao kuzungushwa kwenye baa mbalimbali tena huko nako wengi hawana ajira.

Wanadai lengo la kuwazungusha kwa kuwahamisha kutoka kwenye baa mbalimbali zilizoko miji tofauti ili kuwahamasisha wateja ambao wengi ni wanaume kunywa zaidi huku wamiliki wakijinufaisha zaidi.

Sehemu ya kazi wanatakiwa kuwa na urafiki wa karibu na wateja, anasema mmoja wa wasichana wa baa: “Mwajiri wetu anasema kabisa ikiwa hutaki kumbembeleza mteja, unapaswa kutafuta kazi nyingine.”

Baadhi ya wasichana wanalazimishwa kuingia kwenye ukahaba katika umri mdogo tena wakiwa ni idadi kubwa ya mabinti halafu kwa wakati mmoja.

Ni vyema taasisi kama za ustawi wa jamii, polisi na askari wa ulinzi shirikishi wakafuatilia suala hilo ili kuujua ukweli ili kuwaokoa wasichana hao na kazi ya kutumia kukuza mauzo ya pombe.

Iwapo kuna Chama cha Wafanyakazi wa Mahotelini, Mashambani na Majumbani (CHODAWU) hili linapaswa kuwa jukumu lake la msingi la kutetea na kufuatilia wanachama wake.

Wasichana hawa wanasema wamiliki wanawanyonya na kuwalazimisha tutakutana na wanaume bila ridhaa yao ni udhalilishaji, lakini ni jambo wasilolipenda.

Inabidi utafiti ufanyike kwa sababu serikali inagharamia elimu inakuwaje wasichana hao wasiwe darasani badala yake wafanye kazi kwenye baa mijini?

Aidha ni wakati wa kuzingatia kuwa maradhi mengi yanaambukizwa kupitia ngono na hiyo ni njia mojawapo ya kuwaambukiza watoto hao wadogo magonjwa.

Baadhi ya maradhi yanaweza kuwa ni pamoja na UKIMWI, homa ya ini inayoambukizwa na virusi vya ‘hypatitis’ lakini pia hata maradhi ya saratani ya shingo ya kizazi yanayoambukizwa na Human papilloma virus (HPV), ambayo wakati mwingine husambaa kwa njia ya kujamiiana na watu wengi.

Licha ya serikali kupiga vita madanguro, vitendo kama hivyo kufanyika kwenye baa ni kama kuzigeuza kuwa nyumba za ukahaba ambazo sheria ya Tanzania haiziruhusu.

Suala la wafanyakazi wa baa kutolipwa mishahara nalo linatakiwa kufanyiwa uchunguzi na mamlaka za serikali kama halmashauri, manispaa na TRA kwa upande mwingine kwa kuwa eneo mojawapo linalotozwa ni kodi ya mshahara (pay as you earn) lakini pia kodi ya zuio ambayo kila malipo yanayofanyika hulipiwa kodi.

Ni vyema kuchukua tahadhari na kuokoa wasichana hawa ambao ni mama wa kizazi cha kesho.

HABARI KITAIFA

# Watakaotoa siri Sensa ya Watu na Makazi kufungwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAKARANI wa sensa ya watu na makazi wametakiwa kuwa waadilifu, kutunza siri za kila kaya na watakaokiuka viapo vyao watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufungwa jela. Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi taifa, Anne Makinda, alibainisha hayo jana mkoani hapo wakati akizungumza na viongozi wa dini, serikali, wakurugenzi, watendaji wa kata, maofisa tarafa, Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu, na wadau kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali.

Alisema katika zoezi hilo la kuhesabiwa sensa kutakuwa na usiri mkubwa, makarani watakula kiapo cha kutunza siri za kaya ambazo watapita kuchukua taarifa na watakaotoa siri hizo watafungwa jela.

"Naombeni Watanzania tuonyeshe uzalendo katika zoezi hili la kuhesabiwa sensa na mtoe ushirikiano wa kutosha na kutoa taarifa sahihi, sababu kutakuwa na usiri mkubwa juu ya kuhifadhi taarifa hizo, na karani atakaye toa siri atafungwa jela," alisisitiza Makinda.

Kadhalika, alisema wakati wa zoezi hilo kila Mtanzania atahesabiwa mara moja na kuwataka pia wananchi wasikwepe kuhesabiwa kwasababu ni muhimu kwa maendeleo yao.

Alitaja faida ya sensa kuwa ni serikali kupata idadi kamili ya watu wake, ili kusaidia kupanga mipango yake vizuri ya maendeleo kwa wananchi na kuwapelekea huduma stahiki kulingana na idadi yao.

Katika hatua nyingine Makinda ambaye ni Spika mstaafu, aliwaasa wadau hao wakiwamo viongozi wa dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kuendelea kuhamasisha wananchi washiriki kikamilifu kuhesabiwa kwenye zoezi hilo ambalo mpaka sasa limebakiza siku 49.

Naye Mtakwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Makao Makuu, Pastory Ulimali, alisema taratibu zote za sensa zimeshakamilika, pia utafanyika kwa mfumo wa digitali na hakuna kaya ambayo itaachwa kuhesabiwa kwa sababu ikirukwa mfumo unatoa taarifa.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho walipongeza kupewa elimu ya sensa, huku wakiahidi kutoa ushirikiano wa kuhamasisha wananchi washiriki kikamilifu kuhesabiwa siku hiyo ya Agosti 23, mwaka huu.




Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji (katikati), akipokea zawadi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya GFB Trucks, Imrani Karmal (kushoto), wakati waziri alipotembelea banda lao katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa Sabasaba yanayofanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam jana, kulia ni Mwenyekiti wa Bodi wa kampuni hiyo, Wehbour Karmal. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Miili saba ya waliofariki ajalini yazikwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIILI ya watu saba waliofariki juzi katika ajali iliyohusisha gari na mkokoteni wa ng'ombe, imezikwa jana katika Kijiji cha Lugala, kilichoko Wilaya ya Chamwino, mkoani hapo.

Katika miili hiyo ipo familia ya mama (Helena Mkwawa) na watoto wake Irene Samson na Vaileth Samson, bibi (Eveline Masaka) na mjukuu wake Rehema Yohana na mmoja wa familia nyingine Isack Cherehani.

Ibada ya maziko ilifanyika katika Kanisa la Mtakatifu Marco, wilayani humo.

Akizungumza kuhusu mazishi hayo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Manzase, Charles Kangwe, alisema baada ya ibada mazishi hayo yatafanyika katika makaburi ya kila familia.

Ajali hiyo ilitokea juzi kijijini hapo na kuua watu saba na wengine watano kujeruhiwa baada ya gari kugonga mkokoteni wa ng'ombe uliokuwa umebeba watu 12.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, chanzo cha ajali ni mwendokasi wa dereva wa gari aina ya Toyota Landcruiser lenye namba za usajili STL 9534 ambalo ni mali ya Idara ya Maji Mkoa wa Katavi.

Alisema gari hilo lilikuwa likiendeshwa na Paschal Paulo (29), mkazi wa Katavi na ilikuwa ikitokea Dodoma kuelekea Mtera na kugonga mkokoteni huo.

Kamanda Otieno alisema dereva wa gari hiyo anashikiliwa kwa ajili ya taratibu za kisheria.

Akizungumza kuhusu ajali hiyo, Diwani wa Kata ya Manzase wilayani humo, alisema mkokoteni huo ulikuwa umebeba watu 12 waliokuwa wakienda kwenye mlima wa Lugala kuchimba udongo wanaotumia kufinyanga vyungu.

# Sekta binafsi yatakiwa kuchangamkia fursa kibiashara

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa sekta binafsi za ndani ya nchi kuchangamkia fursa za biashara zinazoletwa nchini kutokana na serikali kufanya jitihada za kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, katika hafla ya utiaji saini wa mikataba ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha nne Tabora hadi Isaka, chenye urefu wa kilometa 165 kati ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) na kampuni za Yape Markez na Korail.

"Lakini niseme wito wangu kwa sekta binafsi, hasa ya ndani, ya nje imechangamka vizuri sana. Kujiweka vizuri ili kunufaika na fursa hizi. Tumepiga kelele kwenye 'local content' (ushiriki wa wazawa), wawekezaji tunajadiliana nao tunakubaliana nao. Lakini inapofika utekelezaji wa 'local content' mashirika ya ndani yanakwenda polepole," alifafanua Rais Samia.

Alisema jukumu la serikali ni kuweka mazingira mazuri, ili sekta binafsi iweze kufanya biashara ikiwamo kufanyia kazi malalamiko mengi yaliyotolewa na sekta hiyo.

Aidha, Rais Samia alimwagiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia upya Sheria ya Ubia wa Sekta Binafsi na ya Umma (PPP) na Sheria ya Manunuzi kwa kuwa zilizopo zinawarudisha nyuma wakati wa kuchagua mwekezaji.

"Tukaiangalie tena sheria yetu ya PPP na sheria yetu ya manunuzi. Hizo sheria wakati mwingine mnafika pahala ambapo mnatakiwa mfanye uamuzi kwa haraka, mnakwenda kwenye 'single source', aliyejitokeza ni mzuri na mnaona mnaweza kwenda naye, mkianza kufanya mnaona shutuma za rushwa zinaanza kujitokeza."

"Dunia ya sasa amekuja mtu, mnaelewana, ana uwezo, mnamwamini mnasaini mnakwenda mbele. Sasa kuanza kuzunguka sijui sheria PPP haikufuatwa, miezi mitatu imepita, minne imepita, mtu na fedha zake anatafuta kwingine kwa kwenda," alisema Rais Samia.

Alisema fedha za kutekeleza ujenzi huo ni mkopo uliotokana na kazi kubwa ya kuzungumza na watu na kuwa ni mali ya Watanzania wote na kuwataka wahakikishe wanausimamia vyema kwa kuwa watawajibika kulilipa deni hilo.

"Kwa hiyo niseme kuwa huu ni uwekezaji mkubwa ambao tumeufanya na niseme kuwa umechangiwa na Watanzania wote kwa sababu huu ni mkopo. Watanzania wote tunakuja kulipa fedha hizi...Hivyo basi tunawajibu wa kuhakikisha tunausimamia vyema," alifafanua Rais.

Vilevile, aliitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kuwa na mipango mizuri ya biashara ya usafirishaji na kuwa ni matumaini ya serikali muda si mrefu safari za Dar es Salaam kwenda Dodoma zitaanza kupitia miundombinu hiyo.

# Shaka: Hitaji la Katiba Mpya ni la Watanzania

Na Maulid Mmbaga

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema upatikanaji wa Katiba Mpya sio la wanasiasa ni la Watanzania na linahitaji mipango mahususi wa kuwashirikisha kikamilifu.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari, alisema CCM haijawahi kubeza na wala kuacha kusikiliza maoni ya Watanzania, huku akisisitiza kuwa chama hicho kinaamini kwamba msingi wa uongozi ni watu na mfumo shirikishi.

"Liko wazi kwamba Katiba hii ni ya wananchi sio ya wanasiasa, lazima mipango iwekwe vizuri kuhakikisha kwamba inapatikana katiba ambayo itashirikisha... iwe ni marekebisho au inaandikwa upya, lakini itapatikana ambayo inatokana na historia ya nchi hii," alisisitiza Shaka.

Alisema anayoyafanya Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye siasa, jamii na uchumi sio utashi wake binafsi bali anaongozwa na maono, dhamira na msingi mkuu wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho.

Alisema miongoni mwa faida zinazotokana na jitihada za serikali ni uwekezaji wenye tija wa mradi wa gesi wa Lindi na Mtwara unaogharimu zaidi Sh. trilioni 70.

Alisema utekelezaji wa mradi huo ni moja ya miradi mikubwa ambayo itasaidia kushusha gharama za maisha kwa Watanzania, kuleta ushindani wa bei na kukuza uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

"Kukamilika kwa mradi ule ni ukombozi kwa Watanzania, katika uongozi wa Rais Samia kazi kubwa imefanyika katika diplomasia ya uchumi na katika kufungua fursa na milango ya kiuchumi, tulikotoka ni kuzuri, tuliko ni kuzuri zaidi na tunakokwenda matarajio ni mazuri zaidi," alisema Shaka.

**CHANGAMOTO YA AJIRA**

Alibainisha kuwa CCM inatambua changamoto iliyoko ya ajira kwa vijana akieleza kwamba jambo hilo sio suala la Tanzania pekee bali ni la dunia nzima na mataifa mengi yanazungumzia ukosefu wa ajira kwa vijana.

"Nataka niwaambie vijana Watanzania bajeti ya mwaka huu imewagusa wananchi, lakini makundi maalum vijana na wanawake, mwelekeo wetu ni kwamba tunataka kufikia lengo ambalo tumeliweka la ajira milioni nane kwa kuhakikisha maeneo yote iwe kwenye miradi ya maendeleo, ya uwekezaji binafsi na ya serikali tutaweka mazingira mazuri ya kuwawezesha kupata ajira," alisema Shaka.



Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), Mkoa wa Kinondoni Dar es Salaam, Tushabe Bebwa (kulia), akimkabidhi cheti mmoja wa wafanyakazi bora kati ya nane kwa mwaka 2022, wa kiwanda cha kutengeneza mabomba ya chuma cha Tanzania Steel Pipe (TSP) kilichoko Ubungo, Joel Mapunda, mwishoni mwa wiki. Mwenye kofia ni Katibu wa TUICO tawi la kiwanda hicho, Mussa Mikemo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bashe atishia kuzifutia leseni kampuni

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ametishia kuzifutia leseni za usajili kampuni zitakazokwenda kinyume na taratibu katika uingizaji na usambazaji wa mbolea kwa wakulima.

Alitoa kauli hiyo jana jijini hapo alipokuwa akizindua usajili wa wakulima na mwongozo wa utoaji wa ruzuku ya mbolea msimu 2022/23.

Alisema kampuni zote zitakazohusika na uagizaji na uingizaji wa mbolea za ruzuku lazima zifuate taratibu za serikali ili kuepuka udanganyifu.

"Sitakuwa tayari kuziangalia kampuni zitakazofanya udanganyifu, nahitaji kuona kila kampuni inafuata kanuni za uagizaji na uingizaji mbolea," alisema Bashe. Katika utoaji ruzuku ya mbolea, alisema serikali itatoa kipaumbele kwa viwanda vya ndani ili kuchochea uwekezaji.

Tayari serikali imeshatoa ruzuku ya Sh. bilioni 59 katika zao la korosho na kwenye mbolea na kuwataka wakulima na wawekezaji wajiandae.

"Naomba niwahakikishie serikali itatoa ruzuku ya mbolea kwa viwanda, tumejipanga kuboresha sekta ya kilimo," alisema Bashe.

Katika hatua nyingine, Bashe aliiomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuondoa adhabu ya kulima kwa wanafunzi aliyekosa, kwa kile alichosema kinamfanya akichukie kilimo akiwa mdogo.

"Agenda 2030 tunahitaji kuona kilimo kinachangia kwa asilimia 10, hivyo kama wizara tunahitaji kujenga vijana wakiwa wadogo kukipenda kilimo," alisema.

Naye Naibu Waziri TAMISEMI, David Silinde, aliwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kufuatilia kwa kina maofisa kilimo kuanzia ngazi ya taifa hadi kijiji wanarudi kufanya majukumu yao ya kitalaamu badala ya kufanya kazi ya kukusanya mapato.

Wanafanya hivyo kwa sababu wanajua maofisa kilimo wengi wanafanya kazi tofauti na taaluma yao ambao imewaweka kazini.

Akifafanua, alisema wanaanza kufuatilia hilo ili kuhakikisha malengo ya Rais Samia Suluhu ya kufanya mabadiliko kwenye sekta ya kilimo yanatimia, pia ajenda ya 2030 sekta ya kilimo ichangie kwa asilimia 10 kwenye Pato la Taifa.

"Ninaomba wakuu wa mikoa na wilaya mkalifuatilie hilo na wizara tutafuatilia kila mahali kuona kama linatekelezeka," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kudhibiti Mbolea nchini (TFRA), Dk. Stephano Ngailo, aliishukuru Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano inayoonyesha katika kuhakikisha mkakati wa usambazaji mbolea unafanikiwa.

# Jela miezi 5 kutishia kuua kwa silaha

Na Ibrahim Yassin, MBOZI

MAHAKAMA ya Mwanzo Vwawa imemhukumu Kilio Nzunda (45) kifungo cha miezi mitano jela au kulipa faini ya Sh. 50,000 na fidia ya Sh. 100,000 baada ya kupatikana na hatia ya kutishia kuua kwa kutumia silaha.

Ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Jeshi la Polisi, Maulid Rashid kuwa Mzunda alitenda kosa hilo Mei 24, mwaka huu, majira ya saa tatu asubuhi katika eneo la Ilembo, wilayani Mbozi kwa kumtishia kumuua na panga, Edward Mapumba (72).

Mtuhumiwa huyo alikana shtaka hilo, huku mashahidi wa upande wa malalamikaji wakieleza walivyoshuhudia, Mapumba akipega kelele za kuomba msaada baada ya kufukuzwa na mtuhumiwa akiwa ameshika panga.

Mashahidi hao walidai, mtuhumiwa alikutwa akikata mahindi ya watu na alipoulizwa alianza kumfukuza mlalamikaji akimtisha kwa panga.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Linah Okello alisema mtuhumiwa alileta shahidi mmoja ambaye ushahidi wake ulionekana kukinzana na mtuhumiwa baada ya kukiri kuwa alipigiwa simu na kupewa taarifa kuwa Nzunda amekamatwa na polisi kwa tuhuma za kutishia kuua.

Alisema alifika nyumbani kwa mtuhumiwa na kukuta akishikiliwa na polisi huku akiwa ameshika panga ambalo alikuwa akilitumia kumfukuzia mlalamikaji kwa lengo la kumkata.

Mahakama hiyo ilimkuta na hatia kwa kitendo alichokifanya kuwa hatarishi kwa jamii, na kutakiwa kulipa faini ya Sh. 50,000 na kumlipa mlalamikaji Sh. 100,000 au kwenda jela miezi mitano.

Wakati huo huo, mkazi wa Ilembo, wilayani hapa, Rord Ernest (25), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Mwanzo kwa tuhuma za kutumia lugha za matusi hadharani.

Ilidaiwa mahakamani hapo jana na Mwendesha Mashtaka wa Polisi mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Okello, kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo Juni 27, mwaka huu, majira ya saa sita mchana, eneo la stendi kuu ya Vwawa kwa kumtukana, Jumbe Mwashitete.

Mshtakiwa alikana kosa hilo na kesi iliahirishwa hadi leo, huku akipelekwa mahabusu kwa kukosa dhamana.

# SUMAJKT kuchangia uzalishaji kukabiliana upungufu mafuta

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Stergomena Tax, amesema kupitia Shirika la Uzalishaji mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), watafanya kazi na wadau katika uchangiaji uzalishaji ili kukabiliana na upungufu wa mafuta ya kula nchini.

Aliyasema hayo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 41 ya SUMAJKT ambayo yamefanyika sambamba na Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea mkoani Dar es Salaam katika viwanja vya Mwalimu Nyerere maarufu Sabasaba.

Akifunga maadhimisho ya miaka 41 ya SUMAJKT, Waziri Tax alisema katika bajeti ya mwaka huu, msisitizo mkubwa umekuwa kwenye sekta ya uzalishaji na moja ya vitu ambavyo vimeongelewa na wadau na wanaweza kuchangia katika kuziba pengo la upungufu wa mafuta ya kula.

"Tutafanya kazi na wadau wengine wakiwamo Wizara ya Kilimo kuona tunaweza kuchangia kwa namna gani katika upungufu huo," alisisitiza.

Alitoa wito kwa SUMAJKT kwa kueleza kuwa, miaka 41 ni mingi na wamefanya mengi, lakini wakati umefika wa kuangalia eneo moja kubwa kuhakikisha wanajipanua na kufika sehemu mbalimbali.

"Hii miradi ya vikosi itaendelea kuwapo, lakini sasa miradi mikubwa ya kitaifa ndiyo maono tunayokwenda nayo. Wakati tukisherehekea miaka 41 ya SUMAJKT tunataka tuchangie zaidi katika uchumi na shughuli za kiuchumi za taifa," alibainisha.

Waziri Tax alisema JKT ipo tayari kushirikiana na mtu yeyote ambaye angependa kupata ujuzi na kusisitiza ubora hasa kwenye vyakula ni kitu muhimu kwa sababu kuna kutengeneza bidhaa nyingi, lakini zikatengenezwa zenye ubora zinazokwenda na matakwa ya kiafya.

"SUMAJKT ipo tayari kwa yeyote na anayependa kuja kupata ujuzi, nitoe wito kwa wafanyabiashara wote, ubora wa bidhaa ni kitu muhimu, kwetu sisi kama walaji, lakini sasa tunataka kwenda kwenye masoko ya nje, utakapokwenda kama bidhaa zako hazina ubora huwezi kupita katika masoko hayo.

"Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya jitihada kubwa anatembea kila wakati kujaribu kututafutia fursa za kibiashara, yeye kazi yake ameifanya, ameshaupiga mwingi, na sisi tuupige mwingi kwa kuhakikisha bidhaa tunazotengeneza zinaingia kwenye hayo masoko na kukubalika.

Alibainisha kuwa biashara ni ushindani na kuna wakati kuna vitu vinafanyika ili mtu asiingie kwenye soko la mtu.

"Lakini, ukikidhi viwango vya ubora itakuwa rahisi kupenya katika masoko hayo tuna kanda huru ya biashara Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na sasa hivi tuna kanda huru ya biashara ya Afrika hizi zote ni fursa, lakini zinahitaji mambo matatu, ubora, kiwango na kufikisha huduma kwa wakati," alisema.

Alisema shirika hilo limejipanga maeneo hayo na kuwataka wafanyabiashara wazawa nao wajipange kuhakikisha wanatimiza hayo matakwa matatu ili waweze kutumia fursa zilizotafutwa na Rais kimataifa.

Pia alitoa wito kwa vijana wanaopata stadi kupitia Jeshi la Kujenga Taifa wazitumie ipasavyo kuanzisha shughuli zao za kiuchumi ili waweze kujitegemea na kuwafundisha wengine ambao hawakupata fursa hiyo.

Alisema katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2022/23, kwenye shirika hilo kuna ongezeko la zaidi ya asilimia 260 katika miradi ya maendeleo ya kimkakati na kuendelea kuweka miundombinu kwa vijana.

Kadhalika, aliishukuru Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kuandaa maonyesho hayo ya biashara mwaka huu yakibebwa na kaulimbiu: "Tanzania ni Mahali Sahihi pa Biashara na Uwekezaji".

Alisema maadhimisho hayo yamewapa fursa SUMAJKT kufanya maonyesho na kuadhimisha miaka 41 tangu shirika hilo lianzishwe mwaka 1981.

Alisema shughuli zinazofanywa na shirika hilo ni za mfano wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi kwa sababu linaendeleza uchumi maeneo mbalimbali.

Pia shirika linakwenda kidigitali zaidi katika kuendesha shughuli za ulinzi.

## RC aagiza mkurugenzi kurudisha mil. 400/- za h'shauri

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel 'amemtwisha zigo' Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Binuru Shekidele, kuhakikisha anarejesha Sh. milioni 400 za mfuko wa Amana ambazo zinatumika kukopesha vijana, wenye ulemavu na wanawake.

Fedha hizo zilitumiwa na halmashauri hiyo kwa matumizi mengine kinyume na maelekezo ya serikali, hatua ambayo imeathiri mfuko wa wanawake, vijana pamoja na watu wenye ulemavu.

Gabriel alisema kuna watu waliokuwa wanakusanya mapato hayo ya serikali na kuweka fedha hizo mifukoni mwao, wanatakiwa kuzirudisha kupitia halmashauri.

Alisema kwa watu watakaokaidi kurudisha pesa hizo watatakiwa kukamatiwa mali zao na kuomba uanze kuandaliwa utaratibu wa kisheria ili kusaidia katika urejeshaji wa pesa za serikali. Aliwataka watumishi wa serikali kuridhika na mishahara yao na kuacha kutegemea pesa zilizotengwa kwa ajili ya makundi maalum.

Baadhi ya wananchi wa wilayani Sengerema walimpongeza Mkuu wa Mkoa kwa kutoa agizo hilo na kwamba fedha kama zilitumika kwa matumizi mengine kinyume na maelezo ya serikali ni makosa. Walisema hali hiyo imeathiri makundi mengine yakiwamo ya vijana, wanawake na wenye ulemavu ambayo yanatakiwa kukopesha fedha hizo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, aliahidi kutekeleza maelekezo yote aliyopewa na Mkuu wa Mkoa.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Nganga, alisema atahakikisha kila mtu aliyehusika na fedha hizo anazirudisha.



Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donnell (wa pili kushoto), akigonga glasi na baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya Barrick katika hafla ya kuadhimisha Siku ya Canada iliyofanyika nyumbani kwa balozi huyo, jijini Dar es Salaam. Barrick ni mmoja wa wadau waliofanikisha hafla hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye ulemavu waona umuhimu sensa kuwapatia haki, maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WATU wenye ulemavu kisiwani Pemba wamesema, sensa ya watu na makazi itasaidia kupunguza changamoto zao na kupata haki zao za msingi, kutokana na kuisaidia serikali kujua idadi halisi na kuwaweka katika mipango ya kimaendeleo.

Wakizungumza na gazeti hili, watu wenye ulemavu na wadau mbalimbali walisema, ipo haja kwa jamii kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu katika sensa, ili waweze kupata haki zao.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wasioona Wilaya ya Chakechake (ZANAB), Suleiman Mansour, alisema watanufaika sana kwa sababu ni agizo la serikali lenye lengo la kujenga, wao watakaposhiriki zoezi hilo itajulikana idadi yao na kutafutiwa mahitaji yao yanayowatosheleza.

"Sisi ni watu wenye mahitaji maalumu, serikali ndio msimamizi wa watu kama sisi, hivyo bila kujua idadi yao halisi watafanya kitu kwa kukisia, jambo ambalo litatuathiri," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa viziwi Wilaya ya Chakechake, Said Omar Said alisema, sensa itasaidia watu wenye ulemavu kwa sababu serikali itakapojua idadi ya watu ni sawa na kujua mahitaji ya binadamu, wanaamini changamoto zinazowakabili zitapata ufumbuzi.

Aliishauri jamii kushirikiana pamoja kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele kushiriki sensa kwa kuwa ni muhimu katika maisha yao.

Anasisitiza wazazi wajitokeze kwa wingi kushirikiana na serikali na kuwatoa watoto wao wahesabiwe, ili kupata haki zao za msingi ya kupata elimu, kujielewa na kujitambua.

Mratibu wa Baraza la Taifa la Watu wenye ulemavu Pemba, Mashavu Juma Mabrouk, alisema kwa kiasi kikubwa watu wenye ulemavu watafaidika na sensa.

Alisema, kupitia sensa serikali itajua wanahitaji vitimwendo vingapi, wasomi wangapi na hata katika masuala ya ajira wanaamini kwamba watapata fursa ya kuajiriwa kutokana na idadi ya wasomi walioko.

Mjumbe kutoka SHIJUWAZA Pemba, Aziza Alawi Mussa alisema, fursa hiyo ya kuhesabiwa kwa watu wenye ulemavu itawasaidia kupata ajira kwalengo la kujikimu.

Alisema kuwa kuna athari mbalimbali inayoweza kujitokeza iwapo watu hao hawatapata fursa ya kuhesabiwa, kwa kuwa serikali haitakuwa na takwimu

sahihi za kupanga mipango yake ya kila siku na hata bajeti haziwezi kwenda sambamba kutokana na kukosa takwimu.

Khalfan Amour Mohamed kutoka Jumuiya ya Watu wenye ulemavu wa akili alisema, sensa inaweza kuwasaidia watu wenye ulemavu katika nyanja tofauti, kwa kuwa itaisaidia serikali katika mipango yake ya kuwaletea maendeleo wananchi wake katika nchi.

Mwananchi Halima Bakar Ali, mkazi wa Wete alisema sensa ni muhimu kwa wananchi wote kwa kuwa inaisaidia serikali kupata taarifa za msingi ambazo zitasaidia kuchapuza maendeleo katika nchi.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepanga kufanya sensa ya watu na makazi Agosti 23, mwaka huu.

# Wajasiriamali wakaribishwa banda la TBS kupata huduma

Habari zote na Elizabeth Zaya

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewataka wajasiriamali na wananchi kwa ujumla kuendelea kutembelea banda lake lililoko kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ili kupata huduma za aina mbalimbali zinazotolewa hapo kwa hapo.

Wito huo ulitolewa jana na Ofisa Uhusiano wa TBS, Neema Mtemvu, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mwitiko mkubwa wa washiriki na wananchi wanaotembelea banda la shirika hilo lililoko kwenye maonyesho hayo yanayofanyika kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Mtemvu alisema maonyesho ya mwaka huu shirika hilo limeshiriki kivingine, huduma nyingi ambazo washiriki na wananchi wanahitaji, wanazipata hapo hapo ikiwa ni pamoja na kusikiliza malalamiko yao na kuyatolea ufafanuzi.

Baadhi ya huduma zinazotolewa kwenye maonyesho hayo na maofisa wa shirika hilo ni pamoja na taratibu za usajili wa bidhaa za vipodozi, usajili wa majengo ya chakula, taratibu za kuthibitisha ubora wa bidhaa na huduma nyingine nyingi zikiwamo za ugezi.

"Washiriki na wananchi wakiwamo wale waliokuwa wanashindwa kufika ofisi zetu kupata huduma kutokana na sababu mbalimbali, wakifika hapa wanazipata, tumejizatiti, tupo kamili watapata huduma zetu," alisema Mtemvu.

Aidha, alisema shirika limeendelea kuthibitisha ubora wa bidhaa za wajasiriamali bure, wanachotakiwa ni kuwa na utambulisho kutoka SIDO.

Alisema bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali zikishapata alama za ubora zinaruhusiwa kuuzwa kwenye masoko ya nchi za Afrika Mashariki bila kulazimika kupimwa tena na hiyo ni kutokana na makubaliano ambayo nchi hizo zimeingia.

"Kwa hiyo wakishapata alama ya ubora watauza bidhaa zao Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Sudani Kusini, kwani tumekubaliana kwamba bidhaa ikiwa na alama ya ubora ya nchi husika haitakiwi kupimwa tena," alisema Mtemvu.

Alisema hiyo fursa kwao ya kuuza bidhaa zao kwenye masoko mengine yakiwamo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Akizungumza gazeti hili kwenye banda hilo, mmoja wa washiriki wa maonyesho hayo, Anarose Itembe, alisema amefurahishwa na huduma zinazotolewa na shirika hilo na kuanzia sasa ataanza mchakato wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zake.

Itembe ambaye ni mjasiriamali alisema awali hakuwa akijua kuwa serikali kupitia TBS imerahisisha kuthibitisha ubora wa bidhaa zao tena bure, akitoka kwenye maonyesho hayo ataenda kuanza mchakato huo.

"Ninawahakikishia TBS nikirudi nyumbani Kibondo nitakuwa balozi mzuri kwa wajasiriamali wenzangu ili tuje TBS kuthibitisha ubora wa bidhaa zetu ili kuweze kuingia kwa kishindo kwenye masoko ya Burundi na DRC," alisema.



Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Nassor Ahmed Mazrui, akipokea zawadi kutoka kwa Ofisa wa Benki ya Akiba, Anthony Kunambi, alipotembelea banda la benki hiyo jana katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba. Waziri ameipongeza benki ya Akiba kwa kuendelea kuwahudumia wafanyabiashara wa kada mbalimbali hapa nchini kwa weledi mkubwa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## VETA kutumia teknolojia mpya kuboresha kazi

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imesema inaendelea kuboresha zaidi teknolojia mpya na kuziingiza kwenye mafunzo vyuo vyake nchini ili kuhakikisha vijana wanaohitimu mafunzo watengeneze bidhaa zinazoingia katika soko la kimataifa.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Peter Maduki, wakati akizungumza kwenye banda la Mamlaka hiyo kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba.

Alisema ili kufanikisha hilo, washirikiana na vyuo vingine vinne vya nje ili kuendesha mafunzo hayo kwa vitendo kupitia teknolojia mpya wanazoboresha.

"Na lengo letu ni kuhakikisha tunatoa wanafunzi bora ambao watatengeneza vitu vyenye viwango vya kutumika sio tu katika soko la ndani, bali na kwenye soko la nje," alisema Maduki.

"Tumeanzisha mfumo na vyuo hivyo kubadilishana wanafunzi, kunakuwa miezi kadhaa ambayo wanakaa darasani na mingine wanakwenda kujifunza nje kwa vitendo."

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi VETA, Anthony Kasole, alisema wamejipanga kuhakikisha wanafunzi wanaotoka katika vyuo hivyo wameiva kwa ajili ya kwenda kutoa huduma sehemu mbalimbali ikiwamo kwenye viwanda.

"Tumekuja kuwaambia Watanzania, wafanyabiashara na wawekezaji kwamba VETA tuko tayari kwa mapinduzi ya viwanda, tumejipanga kutoa wataalamu ambao watakwenda kutoa huduma za uhakika, kwa hiyo wasiogope kuwekeza na kuanzisha viwanda, wataalamu wapo," alisema Kisole.

"Tuna vijana ambao wanafundishwa namna ya kuendesha mitambo mikubwa, kwa hiyo wanafaa na wanatosha kufanya kazi kwenye viwanda vyetu na maeneo mengine, watu wasiogope kuwekeza kwa kuhofia kikosa wataalamu."

## Wanawake wahamasishwa uwekezaji miradi mikubwa

CHAMA cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), kimewashauri wanawake kuchangamkia fursa za uwekezaji kwenye miradi mikubwa badala ya kuwaachia wanaume.

Mwenyekiti wa TWCC, Mercy Sila, alisema hayo wakati akizungumza kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa.

Alisema mara nyingi wanawake wamekuwa wakiogopa kuwekeza katika miradi mikubwa, na kuwahamasisha kuwa imefika wakati wachangamkie fursa hizo kubwa.

"Mazingira ya kufanya biashara Tanzania kwa sasa yameboreshwa sana, hakuna haja ya wanawake kuhofia lolote, ni wao tu kujitoa na kujipanga kuchangamkia fursa," alisema Sila.

"Tunatakiwa tumuunge mkono Rais wetu Samia Suluhu Hassan, kwa kufanya kazi kwa bidii, tusikubali kuwaachia wanaume tu, eti kwa kusema nyingine ni ngumu. Tumeshuhudia wanawake wakifanya mambo mengi makubwa na yanafanikiwa, kwa hiyo hakuna litakalowashinda."

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TWCC, Mwajuma Hamza, alisema wataendelea kutoa elimu kwa wanawake hao kwenye mikoa mbalimbali ili kuwasaidia kufahamu namna ya kuteka fursa mbalimbali zinazojitokeza mbele yao.

"Tumekuwa tukitoa elimu kwa wanawake nchi nzima namna ya kuteka fursa mbalimbali, na kwa sababu hiyo ndiyo kazi yetu hatutachoka, tutaongeza nguvu tuwafikie wote, lengo kubwa ni kuhakikisha hawaogopi chochote kuhusiana na kuwekeza kwenye biashara.

Mabanda ya taka yaliyotishia afya za wananchi





Ukurasa 12

Nipashe
TESA
Jumanne Julai 5, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

**Pinda: Nina mpango na wenye ulemavu, sitawaacha hadi elimu ya juu**

ELIMU NA SABATO KASIKA

USUGU WA AJALI;

# Kamanda ajitosa kuwafunza madereva, abiria kote waliko mkoa kwa mkoa

KIKOSI cha Usalama Barabarani, kimekuwa kikifanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na wimbi la ajali, ikiwamo kuwatoza faini au kuwafungia leseni madereva wanaosababisha ajali hizo ili liwe fundisho kwao na kwa wengine.

Pamoja na juhudi zote zinazofanywa na kikosi hicho ajali za barabarani zikiwamo zinazohusisha mabasi ya abiria zimeendelea kutokea nchini ambapo wakati mwingine zinagharimu maisha ya watu wasio na hatia, kuharibu miundombinu ya barabara na madaraja pamoja na mali hasa magari na majengo.

Kutokana hali hiyo, Kamanda wa kikosi hicho, Wilbroad Mutafungwa, anasema wanajikita zaidi katika utoaji wa elimu kwa madereva na abiria kama njia ya kupunguza ajali hizo.

Kamanda Mutafungwa anasema hayo hivi karibuni, kwenye stendi ya mabasi ya Magufuli iliyoko Mbezi Luis Dar es Salaam, wakati akizindua rasmi utoaji wa elimu hiyo.

Anasema, ajali haina kinga, lakini anafafanua kuwa suala la madereva kuwa makini wawapo barabarani ni la muhimu kuliko methali hiyo, ili hata ajali inapotokea isisababishe madhara makubwa.

"Hivyo ili madereva watambue hilo, tumeona kwamba pamoja na adhabu wanazopata, kuna haja ya kuwapa elimu zaidi ili wale ambao hawataizingatia, basi tupambane nao," Kamanda Mutafungwa anasema.



Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Wilbroad Mutafungwa, akitoa elimu kwa madereva wa mabasi katika stendi ya Magufuli, Mbezi Luis Dar es Salaam kabla ya kuanza safari kwenda mikoani. **PICHA: SABATO KASIKA**

"Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kushirikiana na wadau wake kimeamua kuwekeza katika elimu zaidi kwa madereva, abiria na watembea kwa mguu ili kupunguza ajali, kwani nyingine husababishwa na uzembe," anasema.

### YATAKAYOFUNDISHWA

Katika ufafanuzi wake kuhusu elimu hiyo itakavyotolewa, anasema polisi wa usalama kwa kushirikiana na wadau wengine watakuwa kila stendi kubwa za mabasi nchini, wakiwaelimisha madereva na abiria kabla ya kuanza safari.

"Tuna wadau wakiwamo kampuni ya usambazaji wa magurudumu ya Super doll ambao wako hapa, tunashirikiana kutoa elimu na tunatarajia kutumia vyombo vya habari kutoa hamasa na elimu hii," anasema, akitaja redio, televisheni na magazeti, kuwa ni miongoni mwa vitakavyotumiwa.

Aidha, anataja mkakati wa kuandaa vipeperushi vyenye elimu kuhusu udereva, sambamba na kutumia vyombo vya habari.

Mutafungwa anaeleza kuwa kikosi hicho kinajua kuwa wapo baadhi ya abiria wanaoshabikia madereva wanaoendesha kasi na kwamba ni muhimu watu wa aina hiyo nao waelimishwe, ili wajue madhara ya mwendo huo.

Mkuu wa Ukaguzi wa Magari kutoka makao makuu ya kikosi hicho, Ibrahim Samwix, anawataka madereva kuzingatia udereva wa kujihami, ili kuepuka ajali zinazoweza kuzuilika.

"Udereva wa kujihami ni pamoja na kujilinda ukiendesha ukiona mwenzako anaendesha mwendo ambao haufai na anataka umpishe, fanya hivyo ili asikusababishie ajali, wote mkifanya hivyo ajali zitapungua," Samwix anasema.

Anafafanua kuwa kila dereva akizingatia udereva huo na kuacha mashindano barabarani, atakuwa ameokoa maisha yake na ya abiria wake ambao hutarajia kusafiri na kufika salama kule wanakokwenda.

Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa kampuni ya Super doll, Adam Mubago, anashauri madereva kuepuka kuendesha mabasi yenye matairi yaliyochakaa.

"Yanachangia kusababisha ajali za barabarani, hivyo kila dereva anatakiwa kukagua maguruduni, upepo, breki na vitu vingine muhimu kwenye basi kabla ya kuanza safari, anasema Mubago.

### VYANZO VYA AJALI

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni anasema, utafiti uliofanywa na Chuo Kukuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwa miaka iliyopita, asilimia 76 ya ajali zote husababishwa na vyanzo vya binadamu.

Anataja vyanzo hivyo kuwa ni uzembe, ubovu wa magari ambapo huchangia kwa asilimia nane, huku ubovu wa miundombinu ya barabara ukichangia kwa asilimia 16 ya ajali zinazotokea nchini.

Kutokana na hali hiyo, anasema ni muhimu mabasi na malori kuwa na vidhibiti mwendo na kwamba, nia ya wale wanaoharibu ni kutaka kuvunja sheria, kwa kuwa vifaa hivyo vimewekwa ili kudhibiti mwendo magari yasitembee kwa mwendo usiozidi kilometa 80 kwa

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mabanda ya taka yaliyotishia afya

## • Yageuzwa lulu ni maduka, ofisi binafsi na serikali

ELIMU ya usafi wa mazingira, kuhifadhi taka kwenye madampo ya kisasa na kuhamasisha jamii kubadilika kumezaa matunda na sasa yaliyokuwa mabanda ya kuhifadhia taka au maghuba katika Manispaa ya Shinyanga yamegeuzwa vitega uchumi.

Maghuba hayo yaliyokuwa jirani na makazi ya watu na kugeuka kero majumbani na masokoni, leo yamejengwa na kugeuzwa kuwa maduka na ofisi binafsi na za serikali za mitaa.

Hapo awali mabanda hayo yalijaa taka ambazo hazikuzolewa kwa muda mrefu hata kukaa miezi mitatu na kuhatarisha afya za wananchi hasa baada ya uchafu kuzagaa kwenye makazi yao na kusambaza harufu mbaya, wadudu kama funza na wanyama wakiwamo panya, mbwa na kunguru kutanda kila kona.

Februari mosi mwaka huu gazeti la Nipashe lilichapisha Makala ya kukithiri kwa uchafu kwenye mabanda ya taka katika Manispaa ya Shinyanga na kutishia afya, ikiwa na kichwa. "Ni kichefuchefu mabanda ya taka yakielemewa na uchafu".

Hatua hiyo ilibadilisha hali iliyokuwa huku viongozi wakiimarisha elimu ya usafi wa mazingira ikiwamo kujenga dampo la kisasa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) na Mamlaka ya Maji Shinyanga na Usafi wa Mazingira (SHUWASA).

Dampo hilo lipo Nhelegani na limemaliza adha ya maghuba, Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Manispaa ya Shinyanga, Kuchibanda Snatus, anasema.

Anasema katika kuhifadhi taka hatua kadhaa zinatumika kama uhifadhiwa kwenye mashimo ya kuchimbwa nyumbani, kuziweka vibandani na mwisho kwenye dampo hatua ambayo manispaa hiyo imeifikia.

"Vibanda vyote ya taka katika manispaa hii vilivyokuwa kero kwa wananchi, na wafanyabiashara masokoni, tumevifunga na kuvibadilishia matumizi," anasema Snatus.

"Baadhi ya vibanda hivi vimegeuzwa kuwa maduka pamoja na ofisi za serikali za mitaa, na sasa hakuna kero tena ya uchafu kuhatarisha afya za wananchi,"anaongeza Snatus.

Anafafanua kuwa wananchi na wafanyabiashara kwenye maeneo ya masoko taka wanazozalisha zinahifadhi kwenye mifuko kisha wakala ambaye amepewa kazi ya kuzikusanya hupita na magari na



Ni kibanda cha taka Mtaa wa Mapinduzi kikiwa katika mwonekano wa sasa. Hapo awali kabla ya marekebisho ndivyo taka zilivyokuwa 'zinapamba' eneo hilo. **PICHA: MARCO MADUHU**

> Katika tuzo ambazo hutolewa kila mwaka na Wizara ya Afya, mwaka jana Manispaa ya Shinyanga tulikuwa watano mwaka huu tunataka tuwe namba moja.



kuzizoa kila siku na kuzifikisha dampo.

"Katika tuzo ambazo hutolewa kila mwaka na Wizara ya Afya, mwaka jana Manispaa ya Shinyanga tulikuwa watano mwaka huu tunataka tuwe namba moja. Ni kwa sababu tumeongeza ufanisi kwenye kuzoa taka," anasema Snatus.

Soko kuu la manispaa hiyo ni miongoni mwa masoko yaliyokuwa kero kwa wananchi na wafanyabiashara, kutokana na kuelemewa na taka kwenye vibanda ambavyo havikuzolewa kwa wakati na hata kuziba barabara, lakini hali hiyo imekwisha na sasa mabanda hayo ni maduka.

Mwenyekiti wa Soko hilo, Alex Stephen, anasema mpango huo wa manispaa wa kuondoa vibanda vya kuhifadhia taka wameukubali na sasa wako salama uchafu hauhatarishi afya za wafanyabiashara na wateja.

Anasema wanaendelea kuhamasisha wafanyabiashara kuimarisha usafi wa mazingira pamoja na kutunza taka kwenye mifuko, ili gari la taka likipita wazipeleke na soko kuendelea kuwa safi muda wote.

"Mpango huu wa manispaa kuondoa maghuba kwenye mkazi ya watu na masokoni ni mzuri, lakini natoa ushauri magari ya kukusanya taka hizi yapite kila siku sababu likikosekana hata siku moja hali itakuwa mbaya zaidi tuwe makini tusirudi tulikotoka," anasema Stephen.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Dome kwenye manispaa hiyo, Solomon Najulwa, ambaye ni miongoni mwa wanufaika wa vibanda vya taka kubadilishiwa matumizi, anasema hiyo ni neema kwao na kuondoka kwenye ofisi za kupanga.

Anasema vibanda vya taka kuwa jirani na maeneo ya watu na kusambaza uchafu mitaani ilikuwa kero kubwa kwa wananchi, na walikuwa wakipata wakati mgumu kutatua tatizo hilo, lakini sasa usumbufu huo umekwisha.

"Ninapongeza uongozi wa Manispaa ya Shinyanga kugeuza matumizi ya vibanda hivi vya taka, na sisi serikali ya mtaa wa Dome tumepata ofisi, na tutaanza ujenzi hivi karibuni kwa kushirikiana na wananchi na kuondoka kwenye ofisi za kupanga," anasema Najulwa.

Wananchi ambao wanaishi jirani na vibanda hivyo vya taka nao wanaelezea adha ambayo walikuwa wakiipata awali kabla ya kufungwa na kubadilishiwa matumizi, na kupongeza mabadiliko.

Mwanne Shabani mkazi wa Majengo Makaburini anaelezea adha ambayo walikuwa wakiipata kabla ya vibanda hivyo vya taka kufungwa, kuwa walikuwa wakisumbuliwa na harufu huku uchafu ukizagaa kwenye makazi hayo na kuweka rehani afya zao.

"Mimi naishi jirani kabisa na ghuba la uchafu hili hapa mbele yangu, lilikuwa kero sana kwetu sababu uchafu unajaa na hauzolewi kwa wakati hata miezi mitatu, lakini ni kero unapoanza kurudi na kuzagaa kwenye makazi yetu na kutoa harufu kali," anasema Mwanne.

"Watu walikuwa pia wanatupa mizoga ya wanyama kama mbwa, mifugo kama kuku na ndama huwezi hata kutamani kula chakula, afya zetu zilikuwa hatarini sana na sisi kuumwa matumbo ilikuwa ni jambo la kila leo," anaongeza Mwanne.

Aidha, anasema ilifikia hatua wakatamani kuhamia mahali kwingine kwa muda, hadi pale hali itakapokuwa shwari ili kulinda afya zao hasa watoto ambao huchezea maji ya mvua bila ya kujua yana uchafu na magonjwa ya mlipuko.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, anasema tatizo ambalo lilisababisha vibanda vya taka kuelemewa na uchafu lilitokana na ubovu wa magari yaliyoshindwa kuzizoa.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, anawasisitiza wananchi kuendelea kuimarisha usafi wa mazingira kwenye maeneo yao na kulinda afya zao, na siyo kusubiri hadi wasukumwe na serikali, ili wajikinge na magonjwa ya mlipuko yatokanayo na uchafu.

ELIMU

NA MAULIDI MBAGA

PINDA:

# Nina mpango na wenye ulemavu, sitawaacha hadi elimu ya juu

Wanapotajwa watu na taasisi zinazosimama na watoto wenye mahitaji maalumu, jina la Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, haliepukiki. Kwa kauli yake anasema ana mpango nao, hatawaacha na anawahimiza watu zaidi kujitolea kuwasaidia.

Anasema ameishi na watoto wenye mahitaji maalumu, akiwapa elimu na misaada mbalimbali na miongoni mwao wapo waliohitimu hadi elimu ya juu.

Anashauri kuwaangalia kielimu na kiafya, anapoeleza kuwa suala la tiba ni muhimu kwa hiyo wanahitaji kupata bima ya afya ili kuwasaidia kupata matibabu, wanapopatwa na maradhi.

Mstaafu Pinda anasema watoto wengi wenye ulemavu wanaishi katika mazingira magumu jambo linalowakwamisha kwenye mambo mengi kimaisha.

Anasema hayo kwenye Maadhimisho ya Mtoto Mwenye Ulemavu yaliyofanyika Juni 16 jijini Dar es Salaam, wakati huo akishiriki kuendesha harambee ya kuwachangia fedha za kuwakatia bima ya afya.

Juhudi zake zilizaa matunda na zilikusanya fedha ya bima kwa zaidi ya watoto 500 wenye mahitaji maalumu.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, pamoja na mmoja wa watoto wenye mahitaji maalumu. **PICHA: MAULID MMBAGA**

### TUJIULIZE HAYA

"Nina mpango na watoto wenye ulemavu sitawaacha. Nimeishi nao na nimewasomesha. Wengine wana shahada na hata stashahada, kwahiyo si kisichowezekana kinawezekana, unaweza usifanye kama Pinda, lakini kwa kile kidogo unachoweza kujinyima ukafanya ni thawabu mbele ya Mungu." Anaeleza.

"Sina uhakika wangapi mnajiuliza swali hili kama mimi. Kila ninapomuona mlemavu najiuliza kwanini Mungu aliniumba mimi hivi na huyu hivyo na wote akatuita binadamu? Mara nyingi hilo hatulioni, tusijisahau ...," anakumbusha Pinda.

Ili kuwasaidia watoto Pinda maarufu 'Mtotto wa Mkulima' anasema watatengeneza utaratibu maalumu wa kuchangia mtoto mwenye ulemavu anayehitaji matibabu, akibainisha kuwa bima ya afya ya mtotto kwa mwaka ni Shilingi 50,400.

Pamoja na Pinda, mstaafu Jakaya Kikwete, anaunga mkono kwa kuwachangia fedha ya bima ya afya kwa watoto 100 na kuhimiza watu wajitoe kusaidia wahitaji.

### MIKAKATI YA BALOZI

Balozi wa Watoto Wenye Ulemavu Tanzania, Michelle Mrema, anasema katika mpango wa watoto, wamejitolea kuwasaidia wenye ulemavu wanaotoka kwenye malezi duni.

Anaahidi kuwa watatimiza malengo hayo kwa kuendelea kukusanya fedha kwaajili ya bima za afya, kuongeza ufahamu katika jamii juu ya watoto hao na kuboresha shule zinazohudumia watoto wenye uhitaji maalumu.

"Kama nchi ni lazima tujenge tabia ya kitaifa ya kusaidia watu wenye ulemavu pia niwashukuru wadau wote wanaoendelea kuchangia ili kuwezesha jitihada za kuwawezesha wasiojiweza kuwa katika mazingira bora," anasema Michelle.

### HATUA ZA 'SHIVYAWATA'

Mwenyekiti wa Wanawake na Watoto wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Nuru Awadhi, anasema wamejipanga kusaidia mtoto mwenye ulemavu apate elimu bora kama wengine.

Anasema wanalo jukumu la kushirikiana na serikali na kuhakikisha wanampatia mtoto mwenye ulemavu bima ya afya, akibainisha kuwa Juni 16 mwaka huu wamezindua uchangiaji kupitia simu namba 0689-186463 kwa ajili ya kutekeleza mpango huo na matarajio yao ni kufikia watoto 500.

"Tunaishukuru serikali kwa kuhakikisha mtoto anapata elimu stahiki akiwemo mwenye ulemavu, watoto hawa wana mahitaji mengi maalum sio sawa na mwingine wa kawaida ambaye mzazi wake atanunua peni ya Shilingi 200 na kumpa mtoto akaandikie."

"Hawa wenye ulemavu wengi wanatoka familia masikini wazazi hawana uwezo wa kununua kifaa ambacho kinaweza kumsaidia mtoto mwenye ulemavu kutapa elimu lakini inanunua vifaa hivyo na kuvisambaza shule za msingi na sekondari," anasema Nuru.

### TAASISI BEGA KWA BEGA

Taasisi ya Dk. Reginald Mengi Foundation ambayo imekuwa ikijihusisha na kuwasaidia wenye ulemavu kwa kipindi kirefu ni moja ya wadau ambao wamejitolea kuwasaidia kiafya, uchumi na biashara.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo Shimimana Ntuyabaliwe, anasema ziko fursa mbalimbali za kumsimamia mtoto mwenye ulemavu na kuahidi kutoa 'support' kubwa kwa mtoto mwenye ulemavu na kuongeza kuwa hawatawasahau watoto wengine, wenye mahitaji mbalimbali lakini wana uwezo mkubwa na vipaji vyao vinahitaji kujengwa.

"Vipaji hivi haviwezi kujengwa na mtu mmoja, vinajengwa kuanzia nyumbani lakini vile vile sisi wana jamii kuwapa nyenzo mbalimbali ikiwemo elimu, huduma za afya kwa kuwahakikishia vifaa vya michezo ambayo inakuwa jumuishi inayomfanya mtoto aweze kuchangamana na wenzake," anasema Shimimana.

> Kama nchi ni lazima tujenge tabia ya kitaifa ya kusaidia watu wenye ulemavu pia niwashukuru wadau wote wanaoendelea kuchangia ili kuwezesha jitihada za kuwawezesha wasiojiweza kuwa katika mazingira bora.

### WITO KWA JAMII

Mkurugenzi wa Shirika la Beyond Giving Tanzania, Joseph Msuka, anatoa wito kwa jamii akisisitiza kuwa inapaswa kutambua kuwa mtoto mwenye ulemavu ni sawa na wengine hasa kwenye kupatiwa elimu na huduma za matibabu.

Akizungumza katika siku hiyo, anabainisha kuwa watoto wenye ulemavu wamekuwa wakikabiliwa na vitendo vya kikatili ambavyo vinaanzia ndani ya familia kwenda kwenye jamii huku wakiamiinishwa kwamba mtoto mwenye ulemavu ni mkosi au laana jambo linalohatarisha usalama wao.

Anasema katika shirika hilo wamekuwa wakitoa elimu ya mafunzo kwa watoto wenye ulemavu na kwa wazazi na walezi kuwakatia bima ya afya pamoja na kuifanya jamii itambue haki za msingi za watoto hao.

Mkurugenzi wa Shirika la Action For Community Development (ACODE) Winner Chimba, anasema wamekuwa wanajihusisha na utoaji wa tiba tegemeo kwa watoto wenye ulemavu pamoja na kuwapatia ujuzi wa kazi.

Vile vile Chimba anatoa wito kwa wazazi kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu kwa kuwanyima haki yao ya msingi ya kupata elimu na kuwaona kuwa hawafai akidai kuwa kitendo hicho kinahatarisha maisha yao.

Shangwe Mgaya, Mkurugenzi wa Taasisi ya Living Together Autistic Foundation, anasema moja ya jitihada walizozifanya katika kuwasaidia watoto wenye ulemavu hasa wenye tatizo la Usonji, ni kuwapatia bima ya afya watoto 70 ambao wanahudumiwa tiba ya viungo, kuzungumza, mfumo wa fahamu na tabia.

# Kamanda Mutafungwa ajitosa kuwafunza madereva, abiria waliko mkoa kwa mkoa

INATOKA UK.11

saa.

Ni katika kikao chake na Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, hivi karibuni, akisema madereva wakizingatia sheria ya usalama barabarani kwa kufanya kazi kwa weledi, mfululizo wa jali utadhibitiwa.

Kwa mujibu wa Waziri, takriban watu 1,191 walifariki dunia na 2,139 kujeruhiwa kutokana na ajali za barabarani 1,594 zilizotokea nchini kati ya Julai mwaka 2021 na Machi mwaka 2022.

Anafafanua kuwa kwa mujibu wa takwimu hizo, kumekuwa na ongezeko la ajali za barabarani 366, zikipanda kwa asilimia 29.8 na kwamba ajali nyingi zinasababishwa na uzembe wa madereva, ubovu wa magari na barabara.

Kwamba, polisi waliwafutia leseni madereva 87 na kuwafungia leseni kwa muda vipindi tofauti madereva 141, ikiwa ni adhabu baada ya kuhusishwa na ajali za barabarani.



Mkuu wa Ukaguzi wa Magari kutoka Kikosi cha Usalama Barabarani, ASP Ibrahim Samwix, akizungumza na dereva baada ya kukagua basi lake. **PICHA: SABATO KASIKA**

### CHANGAMOTO ZA KUJIBIWA

Matumizi ya simu barabarani ni tatizo linaloweza kuendelea kusababisha abiria na watumiaji wengine wa barabara kupoteza maisha.

Tanzania haina sheria ya kukataza au kuelekeza namna bora ya matumizi ya simu za mkononi barabarani badala yake madereva wanaongea, kuchati wakiwa kwenye usukani.

Baadhi ya nchi zinakataza dereva kutumia simu barabarani wakati nyingine zinaelekeza kuweka gari pembeni na kusimama.

Aidha, tatizo jingine ambalo halijapatiwa ufumbuzi na linaweza kusababisha ajali ni pamoja na abiria wa mabasi ya mijini au daladala kutokuvaa mikanda badala yake ni dereva pekee ndiye anayelazamika, sheria haimlindi abiria kwenye eneo hili.

Kwa upande mwingine usafiri wa bodaboda, bajaji na daladala unakuwa kero na chanzo cha ajali kutokana na wakati mwingine madereva kufungulia muziki mkubwa unaosababisha wasisikie honi kutoka kwa watumiaji wengine wa barabara.

Hata hivyo, sheria ya usalama barabarani haijaweka wazi namna ya kudhibiti au kumaliza kero ya sauti kali ndani ya vyombo vya muziki.

Suala la kuwabeba watoto kwenye pikipiki nalo linazungumzwa na wadau wanaofuatilia masuala ya usalama barabarani. Ni sahihi kumbeba mtoto kwenye chombo hicho bila kuwa na mkanda wa kumfunga, bila kofia ngumu kichwani, vipi upepo na vumbi kifuani kwake?

Ni masuala ambayo sheria ya usalama barabarani inapaswa kuyatolea majibu kwa kuwa ajali siyo tu itokane na mwendo kasi, uchakavu wa miundombinu, ulevi na kasi barabarani.

## WANENAVYO MALENGA

### MAWIGI KUAZIMANA

Mawigi kuazimana, kumeshamiri kwa sana,
Jinsi watu wapeana, hakuna kuulizana,
Wanawake twawaona, kupendeza washindana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Nywele za bandia sana, watu wengi twawaona,
Mwonekano bora sana, njiani tukipishana,
Kununua wanaona, wanajisumbua sana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.
Siyo pesa nyingi sana, jinsi wanaazimana,
Kwa siku moja peana, buku tano taziona,
Kwa wiki watu wavuna, mifuko yao hutuna,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Magonjwa ambukizana, hayo twaweza yaona,
Mba fangasi kiona, usije shangaa sana,
Wigi kubadilishana, inasababisha sana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Urembo mzuri sana, watu wapendeza sana,
Lakini ni ghali sana, tusije kudanganyana,
Kama wautaka sana, nawe gharamika sana,
Biashara nzuri sana, lakini ina madhara.

Mawigi kuvaliana, na nguo kuazimana,
Hiyo ni hatari sana, yale utayokumbana,
Utashangaa kuona, hata chawa wengi sana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Afya ni muhimu sana, sote tunahimizana,
Wigi si muhimu sana, hasa la kuazimana,
Magonjwa ambukizana, sawa na kuzuliana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Mawigi wapenda sana, yanunue mengi sana,
Mambo ya kungojeana, mpate kuazimana,
Hayo ni mabaya sana, hatari mbele twaona,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Mawigi kukodishana, pesa nyingi kuziona,
Hasara bora kuona, tusijekumalizana,
Bora vingine kuona, si vema kuazimana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Wigi kuazimana, na watu kuchangamana,
Familia utaona, nayo mwaambukizana,
Shida hiyo kubwa sana, acheni kuazimana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### PATRICE LUMUMBA: NI SHUJAA WA AFRIKA

Imetokea habari, jamaa wameandika,
Ya kiongozi mahiri, ambaye twamkumbuka,
Maarufu na jasiri, hapa kwetu Afrika,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Ni Patrice Lumumba, vibaya aliondoka,
Risasi walimlamba, ila hawakutosheka,
Kaburi wakalichimba, ili aweze futika,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Likatwakatwa vipande, aweze kumalizika,
Na hata vile vipande, bado hawakutosheka,
Hofu wao iwapande, tusije kumkumbuka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Kwenye ile tindikali, mwili wakauchomeka,
Uliteketea kweli, lakini hajafutika,
Kwenye moyo na akili, Lumumba twamkumbuka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Bingwa Patrice Lumumba, Kinshasa kwao hakika,
Kupambana hakuyumba, kusema Wazungu toka,
Jinsi alivyowachimba, na wao wakageuka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Mpigania uhuru, sisi tunamkumbuka,
Kwa ukombozi ni nuru, ukoloni kutoweka,
Kweli tunamshukuru, japo alishatoweka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Jino limepatikana, habari imetamka,
Mtu amepatikana, kumuua mhusika,
Jino lake liliona, na hilo akaondoka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Hivi DR ya Congo, ni nani anayefika,
Ambaye kwetu kigongo, mashujaa kufunika?
Bila kusema uongo, Lumumba anafunika,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Jino limepatikana, twazidi kumkumbuka,
Kabla ya kuliona, Lumumba twamkumbuka,
Mitaa utaiona, na majina yatumika,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Afrika twamuenzi, kwa kazi njema hakika,
Kwa majina na utunzi, kazi aliyoishika,
Alikuwa ni kurunzi, Afrika kukomboka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





## WB yaridhishwa maboresho miradi mahakama

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI ya Dunia imepongeza utekelezaji wa mradi wa maboresho ya mahakama ambayo imesema itasaidia wananchi wanyonge kupata haki zao kwa wakati.

Mtaalamu wa Sekta ya Umma kutoka Benki ya Dunia, Christine Owuor, alibainisha hayo jana alipokuwa akifanya mazungumzo na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, yanayolenga kuboresha utendaji wa mahakama.

Kiongozi huyo alisema zaidi ya Sh. bilioni 200 zitatumika katika maboresho hayo na wana matumaini kwamba mahakama ya Tanzania itafanya vizuri kama utekelezaji wake.

Alisema matumaini ya Benki ya Dunia ni kuona wananchi wanyonge wanapata haki zao za msingi kwa wakati na kupongeza matumizi ya teknolojia kwenye usikilizaji wa mashauri mbalimbali.

Kwa upande wake, Prof. Juma, aliihakikishia benki hiyo kuwa Tanzania itanufaika katika mradi huo na haitaiangusha.

Alisema kuwa mafanikio ya mradi wa kwanza wa programu ya maboresho ya mahakama yameipatia Mahakama ya Tanzania tuzo ya heshima katika kutekeleza miradi ya kimahakama ya Benki ya Dunia.

"Malengo ya Benki ya Dunia ni kupambana na umaskini, uwazi na usawa wa kijinsia, ndio maana leo tumepokea ujumbe mkubwa ambao utajiridhisha kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi wetu," alisema Jaji Mkuu.

Jaji Mkuu alisema ujumbe huo utatembelea sehemu mbalimbali ikiwamo kukagua mahakama za aina mbalimbali ili kujiridhisha na utekelezaji wa mradi.

Naye Mkuu wa Kitengo cha maboresho ya mahakama, Dk. Angelo Rumisha ambaye ndiye msimamizi wa mradi, alisema mradi huo ni mkubwa kuliko yote barani Afrika inayotekelezwa.

Alisema katika awamu ya pili inatarajiwa kujengwa Mahakama Kuu katika mikoa na kuongeza idadi ya mahakama za mwanzo katika maeneo mbalimbali nchini.

Aliishukuru benki hiyo kwa kuitambua Tanzania kwa utekelezaji wa maboresho ya mahakama na kuiongezea fedha zaidi katika kutekeleza miradi hiyo.

# Zaidi ya lita 900,000 maji kuzalishwa Bahi

**Na Augusta Njoji,** BAHI

MRADI wa maji wa Bahi unaotekelezwa kwa fedha za Maendeleo ya Ustawi na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, unatarajiwa kuongeza uzalishaji kufikia lita 905,000 kwa siku sawa na asilimia 88.7.

Akizungumza jana kwenye ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilipotembelea mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph, alisema mradi huo utaboresha upatikanaji maji kwa kuongeza lita 528,000 kwa siku sawa na ongezeko la asilimia 51.7, awali zilikuwa zikizalishwa lita 377,000.

Alisema zaidi ya wananchi 17,000 katika maeneo ya Bahi mjini wilayani humo watanufaika na mradi huo.

Pia, alisema serikali kwa kutambua athari za ugonjwa wa UVIKO-19 imetenga fedha za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mfumo wa majisafi eneo la Bahi. Alisema DUWASA ilipokea Sh. milioni 451.5 kutekeleza mradi huo ili kukamilisha na kufikisha maji kwa wananchi, DUWASA kupitia makusanyo yake ya ndani na vyanzo vingine iliongeza Sh. milioni 67.4 kugharamia baadhi ya kazi ili kukamilisha mradi.

"Jumla ya gharama za kutekeleza mradi huo ni Sh. milioni 515.1 ambazo zilitumika katika kazi mbalimbali za mradi, hizo kazi ni utafiti wa maji chini ya ardhi kupata maeneo ya kuchimba visima, ujenzi wa tangi la ujazo wa lita 200,000, ulazaji mabomba ya kusambazia," alisema.

Pia alisema kazi nyingine zilizohusisha mradi huo ni ununuzi na usimikaji mtambo wa kutibia maji, ujenzi wa vibanda vya kuendesha visima, uzio katika tangi, kusogeza umeme na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, aliimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha hizo ambazo zimesaidia upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi.

Naye Mbunge wa Bahi (CCM) Keneth Nollo, alisema mradi huo utasaidia kutatua kero ya uhaba wa maji katika jimbo hilo kutokana na wananchi kutumia maji ambayo sio salama.

Mmoja wa wananchi, mkazi wa Kitongoji cha Chiona wilayani Bahi, Anastazia Yohana, alisema kabla ya mradi huo walikuwa wakilazimika kuamka saa nane usiku kufuata maji na mradi huo ni msaada mkubwa kwao.



Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, akizungumza na wakazi wa mtaa wa Mwaja Kata ya Chamwino baada ya kufanyika kwa usafi juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## JUWAKITA yahamasisha wanawake kushiriki sensa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA), imewataka wanawake nchini kushiriki kikamilifu Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu ili serikali kupata takwimu sahihi.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Taifa, Shamimu Khan, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano wa viongozi wa jumuiya hiyo Kanda E uliofanyika jijini hapa kwa siku mbili.

Khan, alisema wanawake wanapaswa kujitokeza kushiriki sensa ya watu na makazi ambayo imepangwa kufanyika mwezi ujao ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi za kundi hilo na kupanga mipango ya maendeleo.

"Wanawake lazima tujitokeze na tutoe ushirikiano wa kutosha kwa maofisa ambao watakuja siku hiyo kwenye kaya zetu kutuhesabu kwani sensa ni jambo la muhimu sana kwa ustawi wa maisha yetu hata katika vitabu vya dini vimeagiza kufanyika kwa sensa."

"Sensa ni agizo la serikali hivyo hatupaswi kupinga maagizo ya watawala kwani hata vitabu vitakatifu vimetuagiza kuheshimu wenye mamlaka," alisisitiza.

Kadhalika, aliwataka wanawake hao kuwa mstari wa mbele kupinga ndoa za utotoni na mimba katika umri mdogo.

"Wanawake lazima tuelimishane kuhusu vitendo hivi vya ndoa za utotoni na mimba za umri mdogo, lazima watoto wetu wasome kwani vitabu vitakatifu vimetuagiza kuzingatia elimu mtoto wa kike na wa kiume wote wanayo haki ya msingi ya kupata elimu," alisema.

Naye Fatma Mwassa, Mwenyekiti wa jumuiya hiyo Mkoa wa Dodoma, alisema lengo lake kuu ni kulisaidia Baraza Kuu la Waislamu nchini "BAKWATA", kuendeleza uislamu.

Alisema lengo jingine ni kusaidia yatima, wanawake kiuchumi pamoja na kutafuta zaka na sadaka ili kusaidia kundi la wenye uhitaji.

Mwassa, alisema moja ya changamoto zinazoawakabili wanawake wa kiislamu hivi sasa ni utoaji wa talaka kiholela ambao umekuwa ukisababisha wanaume kuoa na kuacha bila sababu za msingi.

"Hivi sasa jambo la utoaji talaka limekuwa jepesi sana hali ambayo inafanya watu kuoa na kuacha kwa wepesi sana tunaomba liangaliwe kwani limekuwa sababu ya kuharibu ustawi wa familia zetu," alisema Mwassa.



# Wakulima warahisishiwa huduma kibenki Chunya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

BENKI ya CRDB imefungua tawi maalumu linalotembea katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya ambalo litakuwa linahudumia wakulima wa tumbaku katika Tarafa ya Kipembawe ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wakulima hao.

Meneja wa CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Jenipher Tondi, alilitambulisha tawi hilo kwa wananchi wa Tarafa ya Kipembawe kwenye mkutano wa hadhara wa kuitambulisha kampuni mpya ya ununuzi wa tumbaku uliofanyika katika Kata ya Lupa Tingatinga.

Alisema pia tawi hilo ambalo ni gari maalumu litakuwa linahudumia wananchi wengine wa kawaida ambao ni wateja wa benki hiyo wakiwamo watumishi wa umma.

Waliamua kupeleka huduma hiyo kutokana na asilimia kubwa ya wakulima wa eneo hilo vikiwamo vyama vya msingi vya wakulima wa tumbaku kuwa wateja wa benki hiyo kwa muda mrefu na kupata shida ya huduma hasa wanapotaka fedha nyingi.

Alisema awali walikuwa wanawahudumia wateja hao kupitia kwa mawakala waliopo katika eneo la Lupa ambao wakati mwingine mitaji yao ni midogo ambayo haitoshelezi mahitaji ya wateja.

"Hili tawi litakuwa linatoa huduma zote za kifedha kama matawi mengine yalivyo ikiwamo kufungua akaunti, kuweka fedha na kutoa na litakuwa linahama kutoka eneo moja kwenda lingine kulingana na mahitaji," alisema Jenipher.

Pia imeboresha huduma zinazotolewa na mawakala kwenye maeneo hayo ili kuhakikisha wakulima wengi zaidi wananufaika.

Alisema benki hiyo imekuwa ikitoa mikopo kwa wakulima wa tumbaku kwa ajili ya kuendesha kilimo cha zao hilo na mpaka sasa limeshatoa mikopo yenye thamani ya Dola za kimarekani milioni 12.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliipongeza benki hiyo kwa kuwasogezea huduma wananchi wa maeneo ya vijijini hasa tarafa hiyo ya Kipembawe ambao kwa muda mrefu walikuwa wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Alisema kabla ya tawi hilo kupelekwa wananchi wa maeneo hayo walikuwa wanasafiri kwenda Makongolosi ama Chunya Mjini ambako ni zaidi ya kilomita 200 hali iliyokuwa ikihatarisha usalama wao.

Aliipongeza pia benki hiyo kwa kuwakopesha fedha wakulima wa tumbaku wilayani humo kwa ajili ya kuendesha kilimo hicho akisisitiza kuwa kilimo hicho kinahitaji msaada mkubwa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Ramadhan Shumbi, aliwataka wakulima kuacha kutembea na fedha nyingi mfukoni ama kuzihifadhi majumbani na badala yake wawe wanazihifadhi benki ambako ndiko kwenye usalama zaidi.

Alizitaka benki zingine kusogeza matawi kwenye maeneo ya wananchi hasa wa vijijini ili kuwaongezea usalama wa fedha zao pamoja na kuwasogezea watumishi na watumiaji wengine wa kifedha huduma.



Wazazi na walezi wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Iyela jijini Mbeya wakiwa kwenye Mkutano wa kujadili nidhamu za watoto wao mwishoni mwa wiki baada ya uongozi wa shule hiyo kuitisha mkutano wa dharura kufuatia wanafunzi hao kuvuta bangi na kuwatishia maisha walimu huku wakiharibu miundombinu ya shule. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

## Wanafunzi sekondari wadaiwa kuvuta bangi, watishia walimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Iyela ya jijini Mbeya, wamedaiwa kuungana na wanafunzi wa shule zingine na vijana wa mitaani kuvuta bangi wakiwa wamevaa sare za shule huku wakiwatishia kuwadhuru walimu.

Mkuu wa shule hiyo, Christopher Kamendu, alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano na wazazi uliofanyika shuleni hapo, alisema wanafunzi hao hutoroka shuleni na kwenda kuvuta bangi kwenye eneo liitwalo 'chimbo'.

Alisema wananunua bangi hizo kutoka kwa vijana wa mitaani ambao wanaungana nao kufanya matukio ya uharifu shuleni baada ya kuvuta ikiwamo kuharibu miundombinu ya shule.

Pia huwatishia maisha walimu wao kwa kuwaandikia ujumbe mbalimbali na kuwatupia kwenye ofisi ya Mkuu shule na maeneo mengine ambayo wanahisi zitaonekana.

Alisema hivi karibuni baadhi ya vijana hao kwa kushirikiana na vijana wa mitaani walivunja ofisi ya nidhamu ya shule hiyo na kuiba nyaraka mbalimbali zikiwamo zinazohusu makosa ya wanafunzi hao hali inayowatia wasiwasi walimu.

"Lakini hawa vijana wa mitaani waliingia hapa na kuwachukua baadhi ya wanafunzi na kwenda nao huko chimbo wakaanza kuwapiga na kuwaloweka kwenye maji na haijulikani sababu iliyowafanya wafanye hivyo," alisema Kamendu.

Mwalimu huyo aliendelea kueleza kuwa vijana hao huwavamia pia walimu wa shule hiyo na kuharibu mali zao huku wakitishia kuchoma shule na nyumba za walimu.

Ofisa Elimu wa Kata ya Iyela, Julius Mgala, alisema baadhi ya wazazi wa wanafunzi hao hawatoi ushirikiano kwa walimu kudhibiti nidhamu za watoto wao hali inayochochea zaidi vitendo hivyo vya uhalifu.

Alilalamikia tabia ya baadhi ya wazazi kutoa taarifa kwa viongozi wa serikali wa ngazi za juu kuhusu adhabu wanazopewa watoto wao wanapofanya makosa shuleni.

Baadhi ya taarifa hizo zinatolewa na wanafunzi hao alisema ni za uongo, lakini wazazi badala ya kwenda kupata ukweli kwa walimu wanapiga simu kwa viongozi wa ngazi za juu.

"Mzazi ukiletewa taarifa na mtoto wako ni vyema ukaja naye hapa shuleni ili uwasikilize walimu, sasa ninyi mkiambiwa mna namba za usalama wa taifa, mawaziri na watu wengine hii hali sio sahihi hata kidogo," alisema Mgala.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Lucy Mpangala, alisema vitendo vinavyofanywa na vijana wa mitaani vya kuwapiga wanafunzi hao na kuwaloweka vinahatarisha maisha na akawataka wazazi kushirikiana na walimu pamoja na bodi hiyo kudhibiti.

Alisema kwa sasa linaweza likaonekana kama ni jambo la kawaida, lakini baadaye inaweza ikaleta madhara zaidi kwa wanafunzi hao kuuawa na wahuni hao.

Alisema baadhi ya wanafunzi wanaovuta bangi hawavuti kwa hiyari yao, wanalazimishwa na wahuni hao wa mitaani jambo ambalo alisema ni hatari.

Ofisa Elimu Taaluma wa Jiji la Mbeya, Joyce Kaguo aliwataka wazazi kufuatilia tabia za watoto wao pamoja na kuwajua marafiki wao ili kuwasaidia pale inapoonekana wanapotoka kitabia.

## Mwandishi wa habari ajitosa kuwania uongozi CCM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWANDISHI wa Habari mkongwe, Charles Mwakipesile amejitosa kuwania nafasi ya Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya.

Mwakipesile alichukua fomu ya kuwania nafasi hiyo juzi ikiwa ni siku ya pili tangu chama hicho kilipotangaza kuanza kutoa fomu kwa makada wake kuomba kuchaguliwa kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu hiyo, Mwakipesile alisema yeye ni mwanachama wa chama hicho kwa muda mrefu na amewahi kukitumikia kwenye nafasi mbalimbali.

Alisema endapo atachaguliwa kushika wadhifa huo, atahakikisha anatumia taaluma zake za uandishi wa habari pamoja na sheria kukisaidia chama hicho tawala hasa kukieneza kwa wananchi.

Alisema kwa muda mrefu wananchi wa Tanzania wamekuwa wakikiamini chama hicho na kukichagua kwenye nafasi mbalimbali na hivyo wanahitaji pia kuimarisha safu za uongozi wa chama ili kuimarisha zaidi imani kwa wananchi.

"Bahati nzuri ni kwamba mimi nimekuwa mwandishi wa habari kwa muda mrefu nakijua vizuri chama, nimeamua kuchukua fomu hii kwa sababu nimetafakari na kujiridhisha kwamba naweza na kwa kuwa chama chetu kina utaratibu wa kupokezana uongozi naamini huu ni wakati wangu," alisema Mwakipesile.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Akwilapo, alisema mpaka siku ya kwanza ya kuchukua fomu hizo ambayo ilikuwa Ijumaa ya wiki iliyopita, makada 23 walichukua za kuomba kuwania nafasi mbalimbali.

Alisema fomu hizo zinatolewa katika Ofisi za Chama hicho za wilaya zote pamoja na Ofisi ya Chama mkoa na Jumuiya zake zote na mwisho wa kuchukua na kurejesha ni Julai 10, mwaka huu.

Aliwataka makada wote wa chama hicho wanaotaka kugombea nafasi zilizotangazwa kujitokeza na kuchukua fomu na wanatakiwa wafuate taratibu za chama hicho ikiwamo kuepuka shamrashamra wakati wa kuchukua na kurejesha fomu.



# Wananchi waelekezwa sehemu ya kupata haki

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amewataka wananchi waitumie Idara ya Katiba na msaada wa kisheria ili kupata haki zao.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria, alisema kuna malalamiko mengi katika jamii kukosa haki zao ikwamo masuala ya udhalilishaji, mirathi, na migogoro ya ardhi na idara kuwasaidia kutatua migogoro hiyo.

Alisema katika kutatua matatizo hayo wanaweza kuitumia idara husika au wawakilishi wao wanaopatikana kwa wilaya zote Unguja na Pemba.

Aidha, alisema idara hiyo itaendelea kuwajengea uwezo wananchi ili kupata haki zao bila ya usumbufu kwa lengo la kuleta maendeleo haraka katika jamii.

Haroun alisema wananchi wana matatizo mengi na kushindwa kuzifikia taasisi husika katika kutetea haki zao, na kueleza kuwa taaluma zaidi inahitajika hasa maeneo ya vijijini ili kujenga uwezo na kuwezesha upatikanaji wa haki.

Hata hivyo, alitaka idara kutoa kipaumbele na kutoa taaluma kwa waandishi wa habari upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi ili kutangaza shughuli za idara kwa lengo la kuleta mwamko kwa jamii na kuripoti changamoto zinazowakabili.

Akizungumzia tatizo la udhalilishaji, alisema bado kuna changamoto kubwa Zanzibar, na kuahidi serikali itaongeza mapambano kwa kasi kubwa ili kuokoa makundi maalumu yakiwamo wanawake na watoto wanaokabiliwa na janga hilo.

Alisema kuwa muhali ni tatizo kubwa katika jamii inayochangia kuongezeka kasi ya vitendo vya udhalilishaji na kuiomba jamii kubadilika.

"Udhalilishaji wa wanawake na watoto imekuwa ni kero kubwa Zanzibar na aibu," alisema waziri huyo.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Taasisi ya msaada wa kisheria Tanzania (LSF), Alphonce Gura, alisema taasisi yake itaendelea kuisaidia Zanzibar katika masuala ya upatikanaji wa haki kisheria hasa makundi maalumu ikiwamo wanawake na watoto.

Aliiomba serikali kupitia Idara ya Katiba na msaada wa kisheria, kuelimisha wananchi sheria zote zilizoko ili kuwasaidia hasa sheria ya biashara na kodi ili kuwajengea uwezo.

Alphonce alisema katika serikali za mitaa bado kuna mwamko mdogo hasa kwa masheha katika masuala ya sheria, alieleza muhimu wa kuwapo kwa msaada huo ili kuondoa malalamiko kwa wananchi wanapokwenda kwa sheha kutaka huduma.

Maadhimisho ya tatu ya wiki ya msaada wa kisheria yanatarajiwa kuadhimishwa Julai 9, mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar Hemed Abdulla na kaulimbiu ni: "Paza sauti jitolee wawakilishe wasio na uwezo".



Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Zanzibar ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa jengo la maduka ya biashara Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui Zanzibar kwa niaba ya Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Uhifadhi bahari unavyochangia uchumi wa buluu

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Uhifadhi wa Bahari, Dk. Makame Omar Makame, amesema uhifadhi wa bahari ndiyo msingi mkuu wa uchumi wa buluu katika kuleta maendeleo nchini kupitia sekta ya uvuvi, utalii na ufugaji wa mazao ya bahari.

Aliyasema hayo Mjini Zanzibar, katika mkutano wa mrejesho kwa wadau wa serikali na wa utalii kuhusu uanzishwaji na utekelezaji wa kazi za uhifadhi wa bahari.

Dk. Makame aliwataka wadau mbalimbali kusimamia uhifadhi wa bahari kutokana na mnyororo mzima wa thamani wa utalii unatokana na mazingira mazuri ya bahari na rasilimali zake.

"Ikiwa tutaathiri maeneo ya hifadhi kutapelekea kuporomoka kwa ajira za vijana kupitia utalii nchini jambo ambalo ni kichochezi cha kuanguka kwa uchumi nchini," alisema.

Dk. Makame alisema idara ipo katika harakati ya kuweka matumbawe bandia kwa ajili ya kurejesha viumbe vilivyoadimika baharini ili kuongeza vivutio na thamani ya utalii.

Naye Ofisa Mkuu wa uhifadhi kutoka Idara ya Uhifadhi wa Bahari, Mohammed Choum, aliwataka wadau mbalimbali na vyombo vya ulinzi na usalama kuwa na ushirikiano wa pamoja katika hifadhi shirikishi na kufanya doria za mara kwa ili kudhibiti uvuvi haramu.

Aliwataka wavuvi kuwa mstari wa mbele kusimamia maeneo ya hifadhi katika kuwadhibiti waharibifu wa rasilimali za bahari kwa ajili ya kuulinda uchumi wa buluu.

Kwa upande wao watembeza watalii, waliiomba Idara ya uhifadhi wa bahari kuwawekea kamati maalumu ya usafi na utunzaji wa mazingira kutokana na uharibifu mkubwa unaotendeka katika hifadhi.

# Washauriwa kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WANANCHI wa Kijiji cha Binguni Mkoa wa Kusini Unguja, wameshauriwa kuanzisha kikundi cha ulinzi shirikishi ili kujikinga na vitendo vya kihalifu vinavyojitokeza katika jamii.

Akizungumza na wakazi wa Shehia hiyo, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Salama Juma Salum, alisema ushirikishwaji wa jamii katika ulinzi shirikishi utasaidia kupunguza vitendo vya kihalifu ambavyo vinashamiri siku hadi siku.

Alisema serikali iko tayari kupambana na vitendo vya kihalifu ikiwamo wizi na utumiaji wa dawa za kulevya jambo ambalo linaathiri familia na jamii kwa ujumla.

Alisema kuwa katika kupambana na vitendo hivyo lazima jamii ishirikiane na serikali kutoa taarifa ikitokea ishara ya vitendo hivyo ili kudhibiti hali hiyo isiendelee kuwapo.

Akifafanua makosa ambayo hayatakiwi kupangiwa sheria ndogo, msaidizi huyo amezitaja ni ubakaji na dawa za kulevya, na baadhi ya watu kutotoa taarifa hizo jambo ambalo linarejesha nyuma jitihada za serikali.

Hata hivyo, aliwashauri wakazi hao kushirikiana kwa pamoja katika ulinzi na kuanzisha sheria ndogo ambazo zitawasaidia kutatua changamoto zinazowakabili na kuanzisha mazizi ya ng'ombe salama ili kujikinga na vitendo hivyo.

Naye Sheha wa Shehia hiyo, Ali Yussuf Mussa, alisema uingiaji wa wageni kiholela unasababisha kujitokeza vitendo vya uhalifu na kuwataka vijana kujitokeza kwa wingi na kujiandikisha kushiriki katika ulinzi shirikishi ili kukabiliana na vitendo hivyo.

Kwa upande wao, wakazi wa shehia hiyo waliomba kupatiwa ulinzi wa doria hasa wakati wa mchana na wanyama wao wanaibiwa kwa wingi katika kipindi hiki cha kuelekea Sikukuu ya Iddi Athhar.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOHN DOUBLE** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S0989-0086** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **KIBARA mwaka 2005** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0128-0683 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **MALANGALI mwaka 2008,**na cheti cha chuo kikuu cha **TUMAINI MAKUMIRA kozi ya LAW** chenye namba ya usajili **TU/M/LLB/08/763** kilichotolewa mwaka **2011.**
**Polisi taarifa KAS/RB/7060/2018**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALALA DAUDI BUYOBE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2115/0111** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI WALLA mwaka 2019.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Polisi taarifa: MWA/NY/RB/254239/2022**

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO 518 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**ELIAMANI OBEL MWAMUGIGA**
**And**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**SARAH OBEL MWAMUGIGA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 1 day of 8, 2022.
**Dated at DAR ES SALAAM this 21 day of 6, 2022.**

.............................

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 71 OF 2022**

In the Matter of the Estate of the Late **JASTINI PASKALI MAGANA**
**By 1. ADELINA HERMAN MZUGE**
**2. .........................................**
All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 06th day of JULY .........2022
**Dated at MOROGO this 17th day of JUNE ...2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**RESIDENT MAGISTRATE**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......36 /2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: SARAH GAUDENSI LIPINGA WA TUMBAKU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: MWAJINA GAUDENSI LIPINGA**

**TANGAZO**
*(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe **14 Mwezi 07 Mwaka 2022** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 01 Mwezi 07 Mwaka 2022**

**HAKIMU**

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA, KANDA YA BUKOBA**
**RUFAA NA. 41/2022, YANAYOTOKANA NA KESI YA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**Na. 236/2010**
**GOSBERT KAHWA.....................MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**MSAFIRI M MALANJA ..............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**Kwa MSAFIRI M. MALANJA Popote ulipo**
Hii ni kukutaarifu kwamba shauri la maombi ya jinai tajwa juu imepangwa kusikilizwa tarehe 03 mwezi Agosti mwaka **2022 saa 3:00** asubuhi, mbele ya Mh. Jaji **NGIGWANA** wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hutohudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo.

**Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 29 mwezi Juni mwaka 2022.**

.............................
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**BUKOBA**

---

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KAHAMA**
**WILAYA YA KAHAMA**

**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA 37 YA 2022**
**MATONGO S/O**
**BUNZARI.......................................MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**DEUS S/O MIHAYO.........................MJIBU RUFAA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: DEUS S/O MIHAYO**
**POPOTE ALIPO.**

Kwa kuwa Muomba rufaa ameleta Rufaa ya Madai,hapa Mahakama ya Wilaya katika Shauri tajwa hapo juu,ambalo litasikilizwa tarehe 20/07/2022.
Unaamuriwa kuhudhuria Mbele ya Mahakama hii manao tarehe 20/07/2022, saa 2:30 asubuhi bila kukosa au kuchelewa, ambapo siku hiyo ni siku ya kusikilizwa kwa Shauri hilo, hivyo unapaswa kuleta utetezi wako au pingamizi la Maombi haya.
Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo, Shauri linaweza kuendelea kusikilizwa na kutolewa hukumu upande mmoja bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama hii leo tarehe 04 Mwezi Julai Mwaka 2022.

.................................
**Donasian J.A**
**HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA KAHAMA**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**
**MISC CIVIL APPLICATION NO. 5 OF 2022**
[Ariginating from civil case NO.97/2018 Resident magistrate's court of Arusha]
**KILIAGRO LIVESTOCK PRODUCTION...DECREE HOLDER**
**VERSUS**
**VICTORIA FINE FOODS COMPANY LTD... 1st J/DEBTOR**
**FARIDA AHMED LUGUSHA...............2nd J/DEBTOR**
**AISHA KOKULAMUKA LUGUSHA............3rd J/DEBTOR**
Notice to show cause why execution should not issue
**[0.xxxi,r.20[1]of the civil procedure code]**

**TO;**
**VICTORIA FINE FOODS COMPANY LTD.**
**FARIDA AHMED LUGUSHA.**
**AISHA KOKULAMUKA LUGUSHA OF BUKOBA.**

Whereas the 'decree holder' has made application to this court for Execution of decree in the above suit,this is to give you notice that you are to appear before this court on the**13th** day of **JULY,2022** to show cause why Execution of Decree should not be issued.

**GIVEN UNDER MY HAND** and the **SEAL** of the court,this **22th day of June,2022**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

.........................................
**PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOHN DOUBLE** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S0989-0086** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **KIBARA mwaka 2005** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0128-0683 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **MALANGALI mwaka 2008,**na cheti cha chuo kikuu cha **TUMAINI MAKUMIRA kozi ya LAW** chenye namba ya usajili **TU/M/LLB/08/763** kilichotolewa mwaka **2011.**
**Polisi taarifa KAS/RB/7060/2018**


---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Shauri la Madai/Ndoa Na 29/2022**
**RICHARD BULLA THOMAS........Mwombaji**
**JOYCE CHARLES MONYI..........Mjibu maombi/Mdaiwa**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
*(Kanuni ya 15(1)(2) ya kanuni za mashauri ya madai Mahakama ya mwanzo)*
**Kwa**
**Joyce Charles Monyi**
**Mkoa wa Katavi**
**Kwa kuwa Mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba/eleza hapa habari za madai)**

**UNAHITAJIKA KUFIKA MAHAKAMA YA MWANZO NJOMBE MJINI**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe ...08... mwezi...07....mwaka ...2022....saa ...2:30AM...asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika ulipokea hati ya kuitwa shaurini ,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
**Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe ...01...mwezi ...07..mwaka ...2022..**

## KUPOTEA KWA VYETI



**EMELDA HELMAN MSIGWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index No. S 2828-0010** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **MOUNT CHAFUKWE SECONDARY SCHOOL mwaka 2012,** Cheti cha ualimu **No. E0513-0028** kilichotolewa na chuo cha ualimu **MANDAKA** . Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/260638/2022.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**KWA HABARI MOTOMOTO**
**USIKOSE GAZETI**
**LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Ukraine yathibitisha Russia kuuteka mji wa Lysychansk

**KYIV,** Ukraine

JESHI la Ukraine limethibitisha kwamba mji wa mashariki wa Lysychansk umetekwa na wanajeshi wa Russia kufuatia vita inayoendelea kati ya nchi hizo mbili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na BBC, Mkuu wa Jeshi la Ukraine alieleza kuwa mji huo ulitekwa baada ya mapigano makali dhidi ya Lysychansk yaliyosababisha vikosi vya ulinzi vya Ukraine kulazimika kujiondoa kwenye nafasi zao.

Waziri wa Ulinzi wa Russia, Sergei Shoigu, alisema vikosi vyake vimeiteka Lysychansk na kuchukua udhibiti kamili wa eneo la Luhansk, baada ya wanajeshi wa Ukraine kuzidiwa.

Mkuu wa majeshi yake alisema kwamba ili kulinda maisha ya watetezi wa Ukraine, uamuzi ulifanywa wa kujiondoa.

**Mkuu wa Jamhuri ya Chechen ya Russia, Ramzan Kadyrov, alitoa ujumbe wa video inayoonyesha wapiganaji wa Chechen katikati mwa Lysychansk.**

Alisema Warussia walikuwa na faida nyingi katika wingi wa silaha, ndege, wafanyikazi na vikosi vingine.

Rais Volodymyr Zelensky aliahidi kwamba vikosi vya Ukraine vitarejea Lysychansk kutokana na mbinu zao na kuongezeka kwa usambazaji wa silaha za kisasa.

Mkuu wa Jamhuri ya Chechen ya Russia, Ramzan Kadyrov, alitoa ujumbe wa video inayoonyesha wapiganaji wa Chechen katikati mwa Lysychansk.

Aidha, kwa upande wa magharibi zaidi, mji unaoshikiliwa na Ukraine wa Sloyansk ulikabiliwa na mashambulizi makubwa ya makombora, huku takriban watu sita wakiuawa, upo katika mkoa wa Donetsk, ambao pamoja na Luhansk zinaunda Donbas yenye viwanda.

Vile vile inasemekana kuwa muda mfupi kabla ya kuzindua vita, Rais wa Russia Vladimir Putin alitambua kuwa mji wa Luhansk na Donetsk ziko huru kutoka kwa Ukraine, ambapo vikosi vinavyoungwa mkono na Russia vilianza uasi mwaka 2014.

Pia taarifa zinasema zaidi ya wiki moja iliyopita wanajeshi wa Urusi waliteka Severodonetsk, jiji lililokuwa na magofu kwa siku kadhaa ya mashambulizi ya Russia. **BBC**



Mwonekano wa jengo lililoharibiwa vibaya katika mji wa mashariki wa Lysychansk nchini Ukraine ambao umetekwa na Russia kutokana na vita inayoendelea baina ya nchi hizo. **PICHA: BBC**

## Papa Francis akanusha madai ya kujiuzulu

**VATCAN,** Italy

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amekanusha madai kwamba anapanga kujiuzulu na kueleza kuwa anapanga kutembelea taifa la Canada mwezi huu na anataraji kuzuru Moscow na Kyiv hivi karibuni ili kushawishi mataifa hayo kusitisha vita.

Pamekuwa na uvumi kuwa Papa Francis, analenga kujiuzulu mwezi Agosti baada ya kukutana na viongozi wa kanisa hilo kujadili katiba mpya ya Vatican, na baadaye kuzuru jiji la Italia la L'Aquila, ambalo linahusishwa na Papa Celestine V, ambaye alijiuzulu upapa mwaka 1294.

Jiji la L'Aquila pia linahusishwa na Papa Benedict wa XVI, aliyezuru jiji hilo miaka minne kabla ya kujiuzulu mwaka 2013, akiwa papa wa kwanza kufanya hivyo baada ya miaka 600.

Papa Francis alisema jana kuwa wazo la yeye kujiuzulu halijamjia na kwamba analenga kutekeleza majukumu yake kama viongozi wengine.

Pia Papa Francis alisema anaweza kulazimika kujiuzulu wadhifa huo wa upapa, iwapo hali yake ya kiafya itamuzuia kutekeleza majukumu yake lakini kwa sasa hana huo mpango.

Kiongozi huyo wa Kanisa Katoliki pia alikanusha uvumi kuwa anaugua saratani na kusema madaktari wake hawajamwambia chochote kuhusu suala hilo, na kusisitiza kuwa goti lake ndilo limekuwa na tatizo ila kwa sasa limepata nafuu.

Papa Francis mwenye umri wa miaka 85, amesisitiza msimamo wake dhidi ya uamuzi wa Mahakama ya Marekani ambao umeruhusu utoaji wa mimba. **RFI**



**Papa Francis mwenye umri wa miaka 85, amesisitiza msimamo wake dhidi ya uamuzi wa Mahakama ya Marekani ambao umeruhusu utoaji wa mimba.**

## Jumuiya ya Kimataifa yaombwa kusaidia kupatikana amani DRC

**KINSHASA,** DRC

KANISA la Katoliki nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) limeiomba Jumuiya ya Kimataifa kusaidia kupatikana kwa amani, Mashariki mwa nchi hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na viongozi wa kanisa hilo jijini Kinshasa katika ibada maalum iliyofanyika kwenye majengo ya bunge, baada ya kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani Papa Francis kuahirisha ziara yake nchini humo kwa sababu za kiafya.

Kiongozi wa Kanisa Katoliki nchini humo Kardinali Fridolin Ambongo, alisema kuwa wakati umewadia kwa makundi ya kujihami kuweka chini silaha na kudhibitiwa haraka, la sivyo taifa hilo litatumbukia katika janga la kibinadamu ambalo halijawahi kushuhudiwa, huku akimtaka Papa Francis kuingilia kati mzozo huo.

Ibada hiyo pia ilihudhuriwa na mwakilishi wa Papa Francis, Kadinali Pietro Parolin, ambaye alisema Papa Francis analiombea taifa la DRC ili liwe na amani, huku akisisitiza sharti makundi ya kujihami yaweke silaha chini.

Pia Papa Francis mwenye umri wa miaka 85 alitoa ujumbe wa mkanda wa video akionyesha masikitiko ya safari yake nchini DRC na Sudan Kusini ilikuwa ifanyike mwezi huu kuahirishwa, huku akiahidi kuzuru mataifa hayo wakati mwingine. **RFI**

## Jeshi Uganda lakanusha kuunga mkono Tigray

**KAMPALA,** UGANDA

JESHI nchini Uganda, limekanusha taarifa ya baadhi ya vyombo vya habari vya Ethiopia, kwamba serikali ya Uganda inaunga mkono waasi wa jimbo la Tigray kuipindua serikali ya waziri mkuu Abiy Ahmed.

Madai hayo ya serikali ya Uganda kuunga mkono waasi wa TPLF yamekuwa yakiripotiwa katika vyombo vya habari vya Ethiopia tangu mwezi Mei, kwamba Uganda inawapa mafunzo waasi wa Tigray, katika eneo la Karamoja, pia kufadhili shughuli za waasi hao kupitia taifa jirani wa Sudan Kusini.

Hata hivyo msemaji wa jeshi la Uganda, UPDF, Felix Kulayigye, alisema madai ya serikali ya Uganda kuwa na njama kuyumbisha serikali ya Ethiopia ni ya uongo na hayana msingi wowote. **RFI**

# MGUNDA 'ROHO NYEUPE' SOPU KUONDOKA COASTAL

**Na Cheji Bakari,** TANGA

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amesema kwake hakuna tatizo lolote kuhusiana na straika wa timu hiyo, Abdul Suleiman 'Sopu' kutakiwa na klabu za Simba, Yanga na Azam FC kwa sababu ni jambo la kawaida kwenye soka.

**Sopu ambaye Jumamo si iliyopita alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mashindano ya Kombe la FA, amekuwa na ki wango kizuri msimu huu uliomalizika.**

Akizungumza na gazeti hili, Mgunda alisema mpira ni maisha na kumzuia mchezaji kwenda kutafuta maslahi ni dhambi.

Mgunda alisema suala la Sopu lilianza kuzungumzwa kwa muda mrefu lakini baada ya kumalizika kwa mechi ya fainali ya Kombe la FA ambapo Coastal Union ilifungwa na Yanga, amepokea ofa kutoka timu mbalimbali.

Alisema kwa mchezaji yeyote wa mpira hiyo ni sehemu yake ya maisha na kawaida baada ya msimu kumalizika, ni haki yake kwenda popote anapoona kuna maslahi.

"Mchezaji kuondoka kwenda timu nyingine hilo suala halizuiliki, timu inatakiwa kumzuia kwa kumpa maslahi kama mnajijua hamna uwezo mnamzuia wa nini? Kwa sababu gani? Ila panaposemwa jambo ujue lipo".

"Mimi kama mwalimu ninayejua hilo katika eneo hilo sipo siwezi kumzuia mchezaji kuondoka kutokana naogopa dhima kwa Mungu, siku ya kiama (mwisho) nitakuja kuulizwa pia mchezaji atakuwekea chuki kwamba wewe ndio sababu ya kuzuia maslahi yake," Mgunda alisema.

Kuhusu mchezaji, Victor Akpan kujiunga na Simba alisema hilo halina ubishi tayari uhamisho wake umekamilika.

"Ni kweli nimepokea ofa nyingi kutoka timu mbalimbali, ila kwa sasa bado sijafanya uamuzi kwa sababu bado kipaumbele changu ni Coastal Union, ila wakishindwa ndio nitajua nitakwenda wapi," alisema Sopu.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Coastal Union, Ahmed Aurora amesema bado wanasubiri ripoti ya Mgunda ili waanze mchakato wa usajili kuelekea msimu ujao.

Aurora alisema watafanya usajili wao kwa siri kwa sababu wanaogopa fitna zinazotawala wakati wa kukamilisha mchakato huo.

Alimtaja nyota ambaye wameshamalizana naye ni raia wa Benin, Olatundi Djibril kwa kumpa mkataba wa miaka miwili.

" Ligi Kuu imeisha hivi karibuni, ni mapema mno kuweka wazi ni wachezaji gani tumewachukua au tunataka kuingia nao makubaliano ya usajili, labda angalau tukiwa katika asilimia 16 tutaweka wazi," alisema Aurora.



Mshambuliaji wa Mburahati FC akimtoka beki wa Ilala FC katika mashindano ya Ligi ya Ufukweni iliyochezwa kwenye ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam juzi. Ilala FC ilishinda mabao 3-2. **PICHA: TFF**

# Zigzag kuzikwa leo Moshi

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Simba aliyefunga bao lililoinusuru kushuka daraja mwaka 1988, John Makelele 'Zigzag', amefariki dunia.

Mwenyekiti wa Umoja wa Maveterani Tanzania, Faza Lusozi, alisema Makelele alifariki Jumamosi katika Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Muhimbili baada ya kuugua saratani ya koo.

Lusozi alisema marehemu ambaye mbali na Simba alizichezea timu za Pamba na Biashara ya Mwanza, ameacha mke na watoto kadhaa, jana aliagwa Muhimbili na kutarajiwa kuzikwa leo Moshi TPC, mkoani Kilimanjaro.

"Alifariki Jumamosi na msiba ulikuwa Bunju A kwa dada yake, tunatarajia kumzika mwenzetu kesho (leo), kusema kweli mpira wa Tanzania umepata pigo kwa kuondokewa na mchezaji mkubwa ambaye aliichezea pia timu ya taifa, Taifa Stars.

Makelele ambaye mashabiki wa soka walimpa jina la 'Zigzag' kutokana na staili yake ya upigaji chenga, pamoja na kasi, alikuwa na uwezo wa kucheza kama mshambuliaji wa kati na winga wa kulia.

Mwaka 1988 aliinusuru Simba kushuka daraja alipofunga bao la pili lililoipa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Yanga.

Ni mechi iliyochezwa Julai 23, 1988 kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Simba ikitakiwa lazima ishinde ili isishuke daraja na Yanga ilihitaji sare tu ili kutwaa ubingwa.

## Mtibwa yafunguka ilipowashika Prisons

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma amesema aliwawekea 'mtego' maalumu wa kuwabana Prisons wanaotumia mtindo wa kucheza mipira mirefu na nguvu ili kuipa timu yake ushindi katika mechi ya kwanza ya mtoano iliyochezwa juzi.

Mtibwa Sugar ilipata ushindi wa mabao 3-1 katika mechi ya mchujo ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya wakati marudiano yatakuwa kesho kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani.

Juma alisema alitengeneza mfumo wa wachezaji wake kukaa nyuma na kushambulia kwa kushtukiza.

"Niliwawekea mtego Prisons kwa sababu wanacheza mipira mirefu na ni watu wa kutumia nguvu, hivyo ukiwa na wachezaji ambao si wavivu wa kukimbizana nao unaweza kuwafunga," alisema kocha huyo.

Straika Jaffar Kibaya ambaye alifunga mabao mawili alisema kocha wake alimuibia siri kuwa mabeki wa kati wa Prisons kiasili si namba yao, hivyo akiongeza kasi na umakini anaweza kufunga mabao mengi.

"Kocha aliniambia Prisons waliweka mabeki wa kati ambao kiasili si namba yao, hivyo kama nikiwa makini na kuongeza mikimbio naweza kuwasumbua na kupata nafasi ya kufunga mabao, na kweli nimefunga mabao mawili," alisema Kibaya.

Kocha Msaidizi wa Prisons, Shaaban Kazumba, alisema wachezaji wake hawakuwa vizuri katika mechi hiyo ingawa walifanya kila kitu sawa na maelekezo yake.

"Tulifanya kila kitu, ila Mtibwa walifanya mashambulizi mawili ya kushtukiza wakapata mabao hayo mawili. Pia wachezaji wangu hawakuwa vizuri leo, ni wakati wa kukaa nao kuwaweka vizuri kisaikolojia," alisema straika huyo wa zamani wa timu hiyo.

Timu itakayopata matokeo mazuri ya jumla itasalia katika Ligi Kuu Tanzania Bara na ile itakayopoteza itakutana na JKT Tanzania inayoshiriki Ligi ya Championship kwenye mechi nyingine mbili za mtoano.



## ZISIKUPITE

### BERNARDO AITAKA BARCA

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ureno, Bernardo Silva, 27, amemwambia wakala wake anataka kujiunga na Barcelona msimu huu wa joto. ***(Sport)***

### PALHINHA KUTUA FULHAM

KLABU ya Fulham imekubali mkataba wa pauni milioni 20 na Sporting Lisbon ili kumfanya kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Palhinha, 26, kuwa mchezaji wao wa kwanza kusajiliwa msimu wa joto. ***(Sky Sports)***

### MARTINEZ AGEUKA LULU

ARSENAL wamepanga kukutana na Ajax wiki ijayo huku vita vya kumsajili beki wao wa Argentina, Lisandro Martinez, 24, ikiendelea. Manchester United wanatajwa wamewasilisha ombi la kumnunua mchezaji huyo. ***(Athletic)***

### POGBA KIMEELEWEKA JUVE

KLABU ya Juventus wiki ijayo itakamilisha usajili wa bila malipo wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba, 29 na winga wa Argentina, Angel di Maria (34), baada ya kuondoka Manchester Utd na Paris St-Germain. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### DE JONG NGOMA NGUMU

MANCHESTER United wamekubaliana malipo na Barcelona kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, lakini bado wanafanya mazungumzo ya nyongeza, na masuala ya kibinafsi bado hayajajadiliwa. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### DE LIGT AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA wamepiga hatua katika jaribio lao la kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt, 22, baada ya Juventus kulegeza msimamo wao kuhusu bei. ***(CBS Sports, Twitter)***

### MILAN, LEEDS VITANI

LEEDS United na AC Milan zinamwania kiungo wa Sassuolo na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Hamed Traore, 22. ***(Corriere dello Sport, via Yorkshire Evening Post)***

### ADAMS ANUKIA LEEDS

LEEDS United pia wameanzisha mazungumzo juu ya kutaka kumsajili kwa pauni milioni 12, kiungo wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Marekani, Tyler Adams, 23. ***(Mail)***

### UNITED, ARSENAL VITANI

KLABU ya Manchester United imeingia kwenye mbio moja na Arsenal kutaka kumsajili Paulo Dybala, 28, ambaye ni mchezaji huru baada ya mkataba wake wa Juventus kumalizika, huku Napoli pia wakimtaka mshambuliaji huyo. ***(La Repubblica, via Star)***

### MCNEIL AGOMBEWA EPL

KLABU ya Crystal Palace inataka kumsajili, Dwight McNeil, 22, kutoka Burnley huku West Ham pia wakivutiwa na winga huyo wa England. Hata hivyo Burnley wanaweza kutaka zaidi ya pauni milioni 10 ambazo klabu hizo za London zitakuwa tayari kulipa. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LAPORTA: BARCELONA HATUMUUZI DE JONG

**Ingawa klabu iko katika changamoto ya kushindwa kumwongezea dau la....**

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amesisitiza klabu hiyo "haina nia" ya kumuuza, Frenkie De Jong anayelengwa na Manchester United, lakini amesema kiungo huyo huenda akakubali kupunguziwa mshahara ili kusalia Camp Nou.

De Jong, ambaye aliibuka kuwa mmoja wa wachezaji motomoto zaidi barani Ulaya chini ya Erik ten Hag katika klabu ya Ajax kabla ya kujiunga na Barca mwaka wa 2019, amekuwa akihusishwa vikali na kuhamia Old Trafford tangu bosi wake wa zamani achukue mikoba ya United.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alisema Mei mwaka huu anapendelea kubaki Camp Nou, ambayo aliita "klabu ya ndoto", lakini matatizo ya kifedha ya Blaugrana hao yamezua uvumi anaweza kuondoka.

**Tamaa ya Barcelona ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski imezidisha tetesi kama hizo, lakini Laporta anaamini De Jong ana furaha katika klabu hiyo na anaweza kusalia ikiwa makubaliano juu ya mshahara wake yatafikiwa.**

"Frenkie de Jong ni mchezaji wa Barca na anatambulika kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani," alisema Laporta akiwaambia waandishi wa habari juzi.

"Tunajua klabu zinazomtaka, sio United pekee, na hatuna nia ya kumuuza ninapata hisia anataka kubaki.

"Yeye yuko vizuri Barca na nitafanya kile ambacho kinawezekana ili Frenkie abaki hapa, lakini ni suala la mshahara linapaswa kurekebishwa.

"Jambo la uhakika ni kwamba viwango vya mishahara vya baadhi ya wachezaji haviendani na viwango vya mishahara ambavyo bodi ya wakurugenzi ninayoiongoza imeweka."

De Jong aliichezea Barcelona mechi 47 msimu wa 2021-22, akifunga mabao manne na kujivunia upigaji pasi bora (asilimia 91.18) kati ya kiungo yeyote wa klabu hiyo.

MECHI KALI
HOME

ANGOLA
2.70 | 3.30 | 2.47
COMOROS

AWAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 274

KUWEKA PESA:
vs PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
vs WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RASHFORD ATAKA MWANZO MPYA



**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford amefichua yuko tayari kwa mwanzo mpya pale Manchester United chini ya kocha, Erik ten Hag.


Rashford alistahimili msimu mgumu wa 2021/22, akifunga mabao matano pekee katika mechi 32 kwenye michuano yote huku United ikimaliza ligi kwa pointi chache zaidi kuwahi kutokea kwenye EPL.

Hii ilisababisha uvumi kuhusiana na fowadi huyo anaweza kuondoka katika klabu yake ya utotoni msimu huu wa joto, lakini 90min inaeleza mchezaji huyo ana nia ya kupigania nafasi yake katika kikosi cha kwanza.

Rashford alirejea kwenye mazoezi ya kujiandaa na msimu hivi karibuni na kufichua alikuwa na nguvu kabla ya msimu ujao.

"Tumepata hisia hizo za msisimko na kelele kwenye uwanja wa mazoezi tena na kwa hivyo ni chanya kwangu kabla ya msimu mpya," alisema akinukuliwa na Daily Mail.

"Katika wiki ya kwanza ya mazoezi tumefanya yote mawili na kila mmoja anatazamia kwenda kwenye ziara na kuweka kile tulichofanya katika mazoezi kwenye michezo ya kwanza.



## *Dybala azigonganisha Man U, Arsenal*

**TURIN,** Italia

ARSENAL na Manchester United zimeingia katika vita moja ya kuwania kumsajili, Paulo Dybala, kwa mujibu wa La Repubblica.

Muda wa Dybala ndani ya Juventus uliisha kwa njia ambayo hakuna upande ambao upo tayari kuendelea kuwa pamoja.

Licha ya kutaka kusalia, Bianconeri hao hawakutaka kumbakisha mshambuliaji huyo wa Argentina, na hivyo kuruhusu mkataba wake kumalizika bila kumwongezea mwingine.

Ripoti zinaonyesha hatarudi tena Serie A bali atakwenda kwenye Ligi Kuu England (EPL), ambapo Arsenal na United zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo.

Huku vigogo hao wa EPL wakiwa tayari kwenye mbio za kumsajili mchezaji mwenzake na Dybala kwenye timu ya taifa ya Argentina, Lisandro Martinez kutoka Ajax, imeripotiwa klabu hizo mbili zimewasiliana na wakala wake, Jorge Antun.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 anapatikana kama mchezaji huru huku mkataba wake na Juventus ukimalizika msimu huu na uhamisho wa kwenda Inter ukikwama baada ya Romelu Lukaku kutua kule.

## HABARI MICHEZO


,002,680

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 06/07/22 | 13:00 | Kashiwa Reysol vs Nagoya Grampus | 2.35 | 2.94 | 2.99 |
| 2. 06/07/22 | 13:00 | Renofa Yamaguchi vs Oita Trinita | 3.15 | 3.05 | 2.20 |
| 3. 06/07/22 | 13:00 | Yokohama F Marinos vs Sanfrecce Hiroshima | 2.20 | 3.25 | 2.95 |
| 4. 06/07/22 | 13:00 | Jubilo Iwata vs Avispa Fukuoka | 2.85 | 2.95 | 2.44 |
| 5. 06/07/22 | 13:00 | Vegalta Sendai vs Ventforet K | 2.28 | 3.10 | 2.95 |
| 6. 06/07/22 | 13:00 | Incheon Utd vs Suwon City | 2.18 | 3.14 | 3.09 |
| 7. 06/07/22 | 13:00 | Suwon Samsung vs Daegu | 2.56 | 3.15 | 2.56 |
| 8. 06/07/22 | 13:00 | Roasso Kumamoto vs Tokushima Vortis | 2.60 | 2.90 | 2.70 |
| 9. 06/07/22 | 13:00 | V Varen Nagasaki vs Montedio Yamagata | 2.21 | 3.09 | 3.09 |
| 10. 06/07/22 | 13:00 | Jeonnam Dragons vs Gyeongnam | 2.70 | 3.10 | 2.46 |
| 11. 06/07/22 | 13:30 | FC Seoul vs Jeonbuk Hyundai | 3.09 | 3.14 | 2.19 |
| 12. 07/07/22 | 19:00 | Grorud IL vs Sandnes Ulf | 2.60 | 3.34 | 2.40 |
| 13. 07/07/22 | 19:00 | Kristiansund vs Tromso | 2.80 | 3.45 | 2.33 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 05 - JULAI 2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1368 | Gwangju vs Bucheon | 1.79 | 3.33 | 4.12 |
| 13:00 | 1991 | Sangju Sangmu vs Jeju Utd | 2.65 | 3.19 | 2.45 |
| 13:00 | 5483 | Seongnam Ilhwa vs Pohang Steelers | 4.32 | 3.44 | 1.73 |
| 13:30 | 2545 | Ulsan Hyundai vs Gangwon | 1.55 | 3.87 | 5.10 |
| 13:30 | 5448 | Daejeon Citizen vs Ansan Greeners | 1.51 | 3.88 | 5.50 |
| 14:30 | 1807 | Preah Khan Reach Svay Rieng FC vs Phnom Penh | 1.82 | 3.79 | 3.49 |
| 14:30 | 2568 | Stirling Lions vs Cockburn City | 1.41 | 4.61 | 5.69 |
| 14:30 | 3518 | Nagacorp FC vs Visakha FC | 4.01 | 4.01 | 1.66 |
| 14:45 | 2562 | Young Lions vs Hougang United | 3.14 | 4.12 | 1.86 |
| 15:00 | 1475 | Seychelles vs Botswana | 9.23 | 4.81 | 1.28 |
| 15:15 | 5252 | Melaka vs Selangor FC | 2.95 | 3.70 | 2.14 |
| 17:00 | 3614 | Sogdiyona Jizzax vs Qizilqum | 1.65 | 3.38 | 5.09 |
| 18:00 | 5304 | Angola vs Comoros | 2.70 | 3.30 | 2.47 |
| 18:00 | 5476 | FC Olimpik vs Navbahor Namangan | 4.92 | 2.81 | 1.85 |
| 19:00 | 4802 | Santos Laguna U20 vs Chivas Guadalajara U20 | 2.01 | 3.43 | 3.23 |
| 19:00 | 5368 | Pyunik Yerevan vs CFR Cluj | 7.18 | 4.19 | 1.43 |
| 20:00 | 1156 | Halmstads BK vs Jonkopings Sodra | 1.44 | 4.68 | 6.51 |
| 20:00 | 1656 | Orgryte IS vs Orebro SK | 2.35 | 3.46 | 2.90 |
| 20:00 | 2883 | Hassania Agadir vs Ittihad Tanger | 1.86 | 3.10 | 4.60 |
| 20:00 | 4451 | Malmo vs Vikingur Reykjavik | 1.21 | 5.78 | 11.95 |
| 20:30 | 5258 | Moghayer AL Sarhan vs Wihdat Amman | 4.93 | 3.65 | 1.61 |
| 20:45 | 5566 | Ludogorets Razgrad vs Sutjeska | 1.17 | 6.41 | 14.03 |
| 21:00 | 2108 | Sindri vs Vaengir Jupiters | 1.68 | 4.20 | 4.00 |
| 21:00 | 2589 | UMF Selfoss vs IF Vestri | 2.03 | 3.74 | 2.95 |
| 21:00 | 2733 | Thor Akureyri vs KV Vesturbaer | 1.63 | 3.89 | 4.33 |
| 21:00 | 2785 | The New Saints vs Linfield Belfast | 1.84 | 3.51 | 3.96 |
| 21:00 | 3375 | Lech Poznan vs Karabakh | 2.11 | 3.30 | 3.30 |
| 21:00 | 4560 | KF Ballkani vs Zalgiris | 2.85 | 3.19 | 2.41 |
| 21:00 | 5755 | DalvikÂk/Reynir vs KFG | 2.17 | 4.20 | 2.65 |
| 21:30 | 3549 | Shamrock Rovers vs Hibernians | 1.29 | 5.19 | 8.99 |
| 21:45 | 1123 | Weston Super Mare vs Exeter | 5.69 | 4.71 | 1.40 |
| 21:45 | 1228 | Workington AFC vs Dumbarton | 2.27 | 3.84 | 2.51 |
| 21:45 | 2551 | Shkupi Skopje vs Lincoln FC | 1.48 | 4.10 | 6.21 |
| 22:00 | 1002 | El Gouna vs Al Ahly Cairo | 8.87 | 4.74 | 1.33 |
| 22:15 | 1975 | HK Kopavogs vs UMF Grindavik | 1.68 | 4.02 | 3.92 |
| 22:15 | 2725 | FH Hafnarfjordur W vs Haukar W | 1.13 | 7.80 | 15.00 |
| 22:15 | 2760 | Throttur Vogum vs Fylkir | 5.89 | 4.81 | 1.38 |
| 22:15 | 3258 | Grotta vs Fjolnir | 2.46 | 3.59 | 2.41 |
| 22:15 | 3319 | KFS vs KH Hlidarendi | 1.55 | 4.71 | 4.12 |
| 22:15 | 3441 | Kari vs IH Hafnarfjordur | 1.47 | 4.93 | 4.63 |
| 22:15 | 4947 | Augnablik W vs Vikingur Reykjavik W | 6.87 | 5.30 | 1.31 |
| 22:15 | 5095 | Afturelding vs Kordrengir | 3.14 | 3.63 | 1.97 |
| 22:15 | 5955 | Ellidi vs Vidir | 2.32 | 4.33 | 2.28 |

### JUMATANO - 06 - JULAI 2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 2239 | Zacatepec vs Tlaxcala FC | 1.76 | 3.39 | 4.23 |
| 01:00 | 3910 | Ituano SP vs Cruzeiro | 3.34 | 2.90 | 2.19 |
| 01:00 | 5195 | Chapecoense vs Londrina PR | 2.14 | 2.89 | 3.48 |
| 01:15 | 1146 | Atletico Mineiro vs SC Emelec | 1.29 | 4.82 | 8.65 |
| 03:30 | 2281 | Boca Juniors vs Corinthians | 1.94 | 3.09 | 3.83 |
| 03:30 | 4399 | Internacional vs Colo Colo | 1.63 | 3.54 | 4.91 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MPOLE AFUNGUKA 2021/22 ULIKUWA MSIMU MCHUNGU

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Geita Gold FC, George Mpole amesema msimu wa 2021/22 uliomalizika hivi karibuni haukuwa rahisi kwake kwa sababu ulikuwa na 'vita' ya kupanda na kushuka hali iliyopelekea azidishe mapambano ili kufikia malengo.

**Geita Gold FC imemaliza msimu ikiwa katika nafasi ya nne kwa kujikusanyia pointi 45 na Mpole akiibuka mfungaji bora baada ya kupachika wavuni mabao 17.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mpole alisema msimu huu ulikuwa na ushindani mkubwa uliobababisha kila timu iliyohitaji kumaliza katika nafasi tatu za juu kupambana.

Mpole alisema wakati msimu unaanza hakujipanga kuwania tuzo ya ufungaji bora lakini alijikuta ameingia kwenye mbio hizo baada ya kufahamu anaweza kutwaa kiatu hicho na anamshukuru Mungu ameibuka mshindi.

"Msimu ulipoanza sikuwaza kuwa mfungaji bora lakini kadri nilivyozidi kufunga, wazo hilo lilinijia na baadaye nikazidi kulifanyia kazi na namshukuru Mungu imetimia," alisema Mpole.

Aliongeza malengo yake makubwa pamoja na wachezaji wenzake ilikuwa ni kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika kila mechi na kumaliza nafasi za juu na hilo wamefanikiwa.

"Kuna mambo mawili ambayo nililazimika kufanya kwanza kuhakikisha timu inapata matokeo, lakini nipambane kufikia malengo, na nilipojiwekea kuwania tuzo ya mfungaji bora ilikuwa lazima nipambane kufikia yote hayo," alisema Mpole.

Alisema amekuwa akipambana zaidi na kujituma katika kila mechi kuhakikisha wanafanikiwa, jambo ambalo limewafanya wawe na msimu wenye mafanikio.



Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Lameck Nyambaya (kushoto), akimkabidhi tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi ya Ufukweni, Abdillahi Mohamed kutoka Ilala FC. Ilala FC ndio ilitwaa ubingwa wa michuano hiyo mwaka huu. **PICHA: TFF**

# *Singida yampa baraka Kiyombo*

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Singida Big Stars umekubali kumwachia mshambuliaji, Habib Kiyombo ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia Simba katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Singida Big Stars iliimtambulisha Kiyombo kuwa mchezaji wao baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili, lakini juzi usiku wametangaza rasmi kuvunja mkataba na mshambuliaji huyo ambaye msimu uliomalizika alikuwa akiitumikia Mbeya Kwanza iliyoshuka daraja msimu huu.

Taarifa za uhakika zilizopatikana jijini zinasema Kiyombo amesaini mkataba wa miaka miwili na Simba na sababu hiyo ndio imepelekea kuvunja makubaliano ya awali aliyoingia na Singida Big Stars.

"Ni kweli Kiyombo amevunja mkataba na Singida Big Stars kwa sababu ya ofa ya Simba, alisaini timu zote mbili lakini ameamua kuchukua uamuzi ya kubaki na mkataba wa Wekundu wa Msimbazi kwa ajili ya msimu ujao," kilisema chanzo chetu.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Singida Big Stars, Hussein Massanza alisema baada ya kupokea barua ya maombi kutoka kwa Kiyombo, walifikia makubaliano hayo kwa pande zote mbili kuzingatia maslahi yake na wao wanamtakia maisha mema huko anapokwenda.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa Mbeya kwanza, Gidion Ngereza alithibitisha nyota huyo amesaini mkataba wa kuitumikia Simba na hati yake ya uhamisho imepelekwa ndani ya klabu hiyo ya Wekundu wa Msimbazi.

# Michezo

Jumanne Julai 5, 2022

Nipashe




'Barca hatumuuzi De Jong' UKURASA 21




Mshambuliaji Abdul Suleiman 'Sopu' (katikati), akisaini mkataba wa miaka mitatu wa kujiunga na Azam FC ya jijini Dar es Salaam inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara. Kushoto ni mmiliki wa timu hiyo, Yussuf Bakhresa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Abdulkarim Amin 'Popat'. **PICHA: SAADA AKIDA**

## Uchaguzi Yanga sasa Jumamosi

**Na Saada Akida**

UCHAGUZI mkuu wa Klabu ya Yanga sasa utafanyika Jumamosi kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere badala ya Jumapili kama ilivyotangazwa hapo awali, imefahamika.

Mwenyekiti wa Kamati ya uchaguzi wa klabu hiyo, Malangwe Mchungahela, alisema sababu za kuurudisha uchaguzi huo kwa siku moja ni kutaka kupisha sherehe za sikukuu ya Eid el Haji ambapo hapa nchini itafanyika Jumapili.

Mchungahela alisema kamati yake imetangaza kufungua dirisha la kampeni kwa wagombea kuanzia jana ambapo mchakato huo wa kuomba kura utakuwa wa siku tano pekee. Kiongozi huyo alisema pia kamati yake imemrejesha kwenye mbio za uchaguzi, Mustafa Himba, ambaye aliondolewa katika mchakato huo baada ya kushinda rufani.

"Himba amerejeshwa baada ya kukata rufani na kamati imejiridhisha na utetezi wake, amefanikiwa kuingia katika mchakato huu wa uchaguzi," alisema Mchungahela.

Alisema jana ilikuwa siku ya mwisho kwa matawi kukabidhi orodha ya viongozi wa watakaopiga kura ili kushiriki uchaguzi huo.

Wanaowania uongozi katika uchaguzi huo ni Hersi Said anayewania urais huku wanaowania cheo cha Makamu Mwenyekiti ni Suma Mwaitenda na Arafat Haji huku Said Kambi, Saad Khimji, Seif Gulamali, Gerard Kilinga, Himba, Seif Rupia, Rispa na Dominus Albinus wanawania nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Utendaji.

Naye Mwenyekiti anayemaliza muda wake, Mshindo Msola amewaomba wanachama wa klabu hiyo kuwa na mshikamano.

# Simba, Yanga chali kwa Sopu

## Straika huyo atua rasmi Azam FC, Yanga ikijipoza kwa Mcameroon...

**Saada Akida na Oscar Assenga,**
TANGA

UONGOZI wa Azam FC umefanikiwa kumsajili mshambuliaji wa Coastal Union ya jijini Tanga, Abdul Suleiman 'Sopu', ambaye alikuwa akiwaniwa na vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa, imeelezwa.

**Sopu ambaye alihusishwa zaidi na tetesi za kutua Simba au Yanga, ndiye Mchezaji Bora wa mashindano ya Kombe la FA yaliyomalizika jijini Arusha juzi.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema Sopu amesaini mkataba wa kuitumikia klabu hiyo yenye makazi yake Chamazi wa miaka mitatu.

Popat alisema klabu hiyo imedhamiria kukiboresha kikosi chake kuelekea msimu mpya kulingana na mahitaji halisi na mapendekezo kutoka katika benchi lao la ufundi na si vinginevyo.

"Kuhusu Sopu hilo limekwisha tayari, ni mchezaji halali wa Azam FC baada ya kuingia makubaliano ya mkataba wa miaka miwili na muda wowote kuanzia sasa tutatambulishwa kwamba msimu ujao atavaa jezi ya Azam," alisema Popat.

Kiongozi huyo alisema wataendelea kuboresha kikosi cha timu hiyo kwa kufanya usajili kwa umakini mkubwa ili msimu ujao wawe bora na kufikia malengo yao ambayo wameshindwa kuyafikia katika msimu uliomalizika.

"Usajili wetu unazingatia mahitaji ya benchi la ufundi kwa kiasi kikubwa na hatutasajili kwa mbwembwe kama wenzetu wanavyofanya, kikubwa mashabiki wetu wawe watulivu kwa sababu msimu ujao tutaingia tukiwa imara zaidi," alisema Popat.

Tayari Azam FC imeshawatambulisha wachezaji wengine watatu wapya ambapo wawili wanatoka nje ya Tanzania ambao ni Kipre Junior, Tape Edinho na Cleophance Mkandala kutoka Dodoma Jiji FC.

***Wakati huo huo***, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wako katika mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Coastal Union, Moubarack Amza, imefahamika.

Chanzo chetu kinadai Yanga ilimchukua Mcameroon huyo jijini Arusha baada ya kumalizika kwa mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa Jumamosi iliyopita.

"Mcameroon hakuwa sehemu ya wachezaji waliopokelea jana (juzi) (Jumapili) katika makao makuu ya timu, na hapo ndipo dalili za kuiacha Coastal zilianza kuonekana, na watu wa karibu walisema ameondoka kikosini," kilisema chanzo chetu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili wa Coastal Union, Ahmed Aurora alisema habari hizo za Yanga kuondoka na mchezaji wao ni za kweli lakini wameitaka timu hiyo kufuata taratibu na kanuni za usajili.

"Kama Yanga wanamtaka wafuate taratibu kwa sababu bado mchezaji huyo ana mkataba na Coastal Union ambao unamalizika Oktoba mwaka huu," Aurora alisema.

Aliongeza Coastal Union iko tayari kukaa mezani na Yanga kwa sababu wanajua mchezaji yuko kazini na anahitaji kufanya kazi sehemu yenye maslahi bora kwake.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042